# SITIARI, JAZANDA NA MWINGILIANOMATINI KATIKA *NAGONA* NA *MZINGILE*

NA

JANE MORAA OCHOKI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA "MASTER OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library
0496783 2

2005

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote

..................................................................

Jane M. Ochoki

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya Chuo Kikuu

..................................................................

Dkt. K.W Wamitila

..................................................................

Dkt. Kineene wa Mutiso

# TABARUKU

Kwa mamangu mzazi Priscah aliyenilea na kunisomesha

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani kwa baadhi ya watu ambao bila mchango wao na uvumilivu wao mwingi, kazi hii haingeweza kufanyika kikamilifu.

Kwanza kabisa nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. K. W. Wamitila na Dkt. Kineene wa Mutiso kwa ushauri na mawazo yao waliyonipa hadi nilipomaliza kuiandika tasnifu hii. Maoni na mwongozo wao ulinitia moyo kuendelea na kazi hii hadi tamati yake.

Aidha ninawashukuru wahadhiri wengine wa somo la Kiswahili katika Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika. Ningependa kuwashukuru Dkt. Kithaka wa Mberia, Prof. Abdulaziz, Marehemu Bw. Richard Mgullu, Bw. T. Arege, Dkt. Tom Olali na Dkt. Mwenda Mbatiah. Wahadhiri hawa walinisaidia si haba kwa kunifunza na hata kila nilipohitaji vitabu hawakusita kuniazima.

Sitasahau kuwashukuru wanafunzi wenzangu Sarah Ndanu, Sussy Nandama, Eunice Nangira, Mutua, Evans Bogonko na Kahiro kwa ushirikiano wao pamoja na moyo wa kujitolea uliniondolea tewengu mara kwa mara.

Sitasahau kuwashukuru wafuatao kwa misaada yao ya aina mbalimbali iliyonisaidioa kufanikisha masomo yangu: Kanzika na Assumpta.

Hatimaye ningependa kuwashukuru watoto wangu Jonathan, Linda na Brian waliovumilia muda wote wa masomo yangu bila kuchoka hata nilipolazimika kutokuwepo nyumbani ili kushughulikia masomo yangu.

# MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia sitiari, jazanda na mwingilianomatini katika riwaya mbili za Kezilahabi: ***Nagona*** na ***Mzingile***. Tasnifu yenyewe ina sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumelielezea tatizo la utafiti, madhumuni ya kazi hii, sababu za kuchagua mada hii na mipaka ya kazi hii. Aidha tumefanyia udurusu yale yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Nadharia tulizotumia katika kazi hizi ni Umuundoleo na Umwingilianomatini.

Katika sura ya pili tumeshughulikia kwa ufupi kazi za Kezilahabi za kinathari zilizotangulia ***Nagona*** na ***Mzingile*** kwa nia ya kuzilinganisha na kuzitofautisha kimaudhui na kimtindo. Sura ya tatu imejadili matumizi ya sitiari na jazanda katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** na vile fani hizi zimesaidia kufanikisha maudhui ya kazi hizi.

Sura ya nne imeonyesha vile ambavyo kuna mwingiliano wa kimatini baina ya riwaya hizi mbili na fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia riwaya ya ***Pedro Paramo*** na ***Babu Alipofufuka.***

Hatimaye tumehitimisha kazi hii katika sura ya tano ambapo pia tumetoa mapendekezo kuhusu sehemu ambazo zinaweza kufanyiwa tahakiki siku zijazo hasa upande wa fani.

## YALIYOMO


Ungamo i

Tabaruku ii

Shukrani iii

Yaliyomo iv

Muhtasari vi

**SURA YA KWANZA**

1.1 Tatizo linalofanyiwa utafiti.................................................... 1

1.2 Nadharia tete.......................................................... 2

1.3 Madhumuni ya tasnifu.................................................2

1.4 Sababu za kuchagua mada,.............................................. 3

1.5 Mipaka na upeo wa tasnifu.............................................. 4

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii........................................ 4

1.7 Msingi wa kinadharia.................................................. 5

1.8 Njia za utafiti.......................................................... 8

**SURA YA PILI**

Kazi za kinathari za Kezilahabi zilizotangulia Nagona na Mzingile

2.1 Utangulizi...........................................................9

2.2 Rosa Mistika.......................................................... 9

2.3 Kichwamaji............................................... .......11

2.4 Dunia Uwanja wa Fujo..............................................14

2.5 Gamba la Nyoka........................................................ 16

2.6 Hitimisho............................................................. 18

**SURA YA TATU**

Sitiari na jazanda katika Nagona na Mzingile

3.1 Utangulizi........................................................................20

3.2 Nagona na Mzingile.............................................................. 21

3.3 Sitiari zinazouakisi ukweli....................................................31

3.4 Hitimisho.............................................................................35

**SURA YA NNE**

Mwingilianomatini katika Nagona na Mzingile

4.1 Utangulizi.........................................................................36

4.2 Kuingiliana kwa Nagona na Mzingile na fasihi simulizi................... 37

4.3 Nagona, Mzingile na Pedro Paramo ......................................... 43

4.4 Dini..................................................................................... 49

4.5 Usawiri wa wahusika na mazingira........................................... 52

4.6 Mbinu nyingine za ki-Usasaleo na Umuundoleo...........................57

4.7 Hitimisho............................................................................. 58

**SURA YA TANO**

Hitimisho

5.1 Muhtasari wa mambo muhimu............................................... 59

5.2 Mapendekezo......................................................................... 62

Marejeleo ............................................................................. 64

# SURA YA KWANZA

## 1.1 TATIZO LINALOFANYIWA UTAFITI

Katika kazi hii tumezihakiki riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi yaani ***Nagona*** na ***Mzingile*** kwa kuzilinganisha na kuzitofautisha na kazi zake za kinathari za awali kama vile ***Rosa Mistika*** (1971), ***Kichwamaji*** (1974) ***Gamba la Nyoka*** (1979) na ***Dunia Uwanja wa Fujo*** (1981).

Katika uhakiki wetu tunatarajia kuchunguza maendeleo ya Kezilahabi hasa upande wa maudhui, baadhi ya fani kama vile sitiari, jazanda na mwingilianomatini. Hii ndiyo sababu tumetumia sehemu hii kama kitangulizi ili kuyachunguza maendeleo hayo.

Tumechagua mada hii kwa kuwa riwaya hizi hazijawahi kufanyiwa uhakiki kwa mwelekeo sawa na ule ambao tumechukua wa kuchunguza kazi hizi hasa upande wa fani. Riwaya hizi zimewahi kufanyiwa tahakiki na wahakiki wengine kama vile: C.I Mungah (1999), M. Mbatiah (1997) na K. W. Wamitila. (1997).

Wahakiki hawa hasa Mungah amehakiki riwaya hizi kwa msingi wa nadharia ya kisosholojia. Kwa maoni yetu, kuhakiki riwaya hizi mbili kwa msingi wa nadharia hii ambayo kulingana na Mungah huonyesha vile fasihi inavyoakisi vipengele vya maisha katika jamii, kutamaanisha kuwa baadhi ya vipengele vya kazi hizi vitakuwa vigumu kuainishika. Kwa mfano, usawiri wa wahusika na mandhari katika kazi hizi ambao umekiuka kile ambacho tunaweza kukiita uhalisi wa jamii au mazingira.

Aidha nadharia aliyotumia Mungah haimwezeshi kabisa kuchunguza fani kwa kuwa mkazo wake upo zaidi katika upande wa maudhui.

Katika *Nagona* na *Mzingile* mwandishi amedhihirisha uwezo wake wa kufinyanga lugha ndiposa tukatumia nadharia ya Umuundoleo katika kuzihakiki kazi hizi mbili. Aidha tumeitumia nadharia ya mwingilianomatini.

## 1.2. NADHARIA TETE

a) Riwaya za *Nagona* na *Mzingile* zimeingia katika mkondo mpya wa kimaandishi.

b) Matini za kifasihi huchangizana kimaudhui na kimtindo.

## 1.3 MADHUMUNI YA TASNIFU

Katika kazi hii tumechunguza jinsi ambavyo *Nagona* na *Mzingile* zimeingiliana na kutofautiana na kazi nyinginezo za Kezilahabi za kinathari hasa vile ambavyo mtazamo wake kuhusu maisha umejitokeza katika kazi hizi zote.

Pili, tumeangalia jinsi ambavyo mwandishi ametumia lugha kufanikisha maudhui yake. Hapa tumeangalia zaidi matumizi ya sitiari na jazanda katika kazi hizi mbili. Suala hili tumelichunguza kwa kuzingatia nadharia ya Umuundoleo ambapo lugha imeangaliwa kama jira (axis) na maana halisi zinazowezakana, mipangilio ya kijamii pamoja na matokeo yake imeelezwa.

Tatu, tutaliangalia suala la umwingilianomatini ambalo pia limefumbatwa na nadharia hii ya umuundoleo kwa kuwa lugha bado imetumika kama jira ambapo maana halisi zimejitokeza hasa kwa baadhi ya mambo ambayo ni bia. Baadhi ya mambo haya ni masuala ya kifalsafa kama vile maana ya maisha, maarifa, kifo na hata nafasi ya dini ambayo ni baadhi ya masuala yaliyoshughulikiwa katika tasnifu hii.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Dhamira ya kuihakiki kazi yoyote ya fasihi ni kuweka mawazo yaliyomo katika maelezo sahili ili ieleweke kwa uwazi zaidi. Riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** ni kazi za kimajaribio. Utafiti huu una lengo la kutoa mchango katika kuelewa kazi hizi zaidi.

Kezilahabi ni mwandishi ambaye amebobea katika uwanja wa fasihi na katika riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** ametumia mtindo wa kimajaribio ambapo ametumia usimulizi usio wa moja kwa moja, mpangilio wa vitushi (msuko) uliovurugika ambapo kuna ukosefu wa mfuatano wa vitushi, kuna matumizi mapana ya sitiari na vile vile mwingilianomatini upande wa dhamira, motifu na visasili. Hizi zote ni elementi za Usasa na Usasaleo.

Kwa kuwa wahakiki waliotutangulia kama vile B. T. Wambui (1992) na C. I Mungah (1999) walitumia mtazamo tofauti hasa ambao haungeelezea kwa nini muundo wa kazi hizi umetofautiana na kazi nyingine za Kezilahabi basi tumeonelea kuwa tuchukue mwelekeo huu. Mungah anasema katika tasnifu yake kuwa Kezilahabi amelipa suala la maisha mtazamo tofauti na riwaya za

hapo awali na kwa kuangalia maisha kwa njia ya kifalsafa. Anasema kuwa kwa kufanya hivi amedhihirisha kupevuka kwake kisanaa na kimawazo.

Maelezo ya Mungah hayamuliki kwa undani sababu hasa zinazozitofautisha kazi hizi na zile nyingine za Kezilahabi kama nilivyoelezea hapo juu. Hivyo, ni wazi kuwa wengi wa hawa wahakiki wamehakiki ***Nagona*** na ***Mzingile*** upande wa maudhui tofauti na vile tumefanya katika tasnifu hii.

## 1.5 MIPAKA NA UPEO WA TASNIFU

Tutajikita zaidi katika riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile.*** Tutazilinganisha riwaya hizi na riwaya zake (Kezilahabi) nyingine ambazo ni ***Rosa Mistika*** (1971), ***Kichwamaji*** (1974), ***Gamba la Nyoka*** (1979) na ***Dunia Uwanja wa Fujo*** (1981).

Aidha tutahakiki matumizi ya sitiari na jazanda na mchango wa fani hizi katika kukuza dhamira ya kazi hizi. Hatimaye tutadhihirisha jinsi ambavyo matini za kifasihi huingiliana hasa upande wa fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia visasili na riwaya ya ***Pedro Paramo*** na ***Babu Alipofufuka.***

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** zimefanyiwa uhakiki na wahakiki wengi ambao baadhi yao wameyashughulikia maudhui ya kazi hizi hasa motifu ya maisha katika tahakiki hizi, suala la fani limepitiwa kijuujuu tu na hivyo

tumeshughulikia suala hili katika tasnifu hii kwa nia ya kuonyesha vile limetoa mchango mkubwa kwa maana ya kazi hizi

Mbali na haya, nadharia walizotumia wahakiki hawa hasa nadharia ya kisosholojia aliyotumia Mungah ambayo inatathmini motifu ya maisha kuwa ni zao la jamii alimokulia mwandishi inashindwa kuelezea yale mandhari ambayo bila shaka ni ya kifantasia.Waandishi wengine ambao wamechangia katika uhakiki wa kazi hizi ni kama vile M. Mbatiah, L. A Mbughuni, M. Msokile na K.Wamitila. Hawa nao wamezihakiki kazi hizi zaidi upande wa maudhui.

Kazi hizi ***(Nagona*** na ***Mzingile***) hazijapata kuangaliwa kwa kina upande wa mtindo au fani hasa kwa muktadha wa Umuundoleo, Usasa na Usasaleo kama tumefanya katika utafiti huu. Katika utafiti wetu tutaonyesha umuhimu wa lugha katika kuunda maana na kwamba lugha ndiyo hujenga dhamira.

## 1:7 MSINGI WA KINADHARIA.

Nadharia ambazo zitaongoza uhakiki wetu ni Umuundoleo na Umwingilianomatini. Umuumndoleo kulingana na Cuddon ni dhana inayoelezea mikabala tofauti ya kifasihi, kifalsafa na nyinginezo kwa kusisitiza wajibu wa lugha katika kuzua maana tofauti tofauti.

Nadharia ya Umuundoleo hupinga mtazamo unaodai kuwa kuna ukweli fulani katika matini za kifasihi na inatia mkazo zaidi kwa msomaji ambaye anaweza kutoa maana mbalimbali zinazoweza kutokana na matini za kifasihi. Aidha nadharia hii inatuwezesha kuelezea kwa upevu namna

ambavyo sifa za urasimi za kiutunzi za riwaya kama vile usimulizi, hadithi, suala la uumbaji na usawiri wa wahusika, mandhari na msuko zimekiukwa ili kusuka ile dhamira ya jinsi ulimwengu ulivyo na kwa hali hii inaonyesha jinsi ambavyo maana imo kwenye lugha.

Dhamira nyingine ya kuangalia kazi hizi kwa mwelekeo huu ni kuonyesha zile elementi za kazi hizi ambazo ni za Usasa na Usasaleo. Tunaona kuwa katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** mwandishi amejitenga kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa kirasimi. Kuna kukatizwa kwa mkondo wa usimulizi, usawiri wa mandhari si wa kiuhalisia aidha mwandishi ametumia sitiari na jazanda kochokocho katika kazi hizi mbili kwa hali hii tunashuhudia jinsi ambavyo lugha imekuza dhamira ya kazi hizi.

Katika nadharia hii, wana-Umuundoleo wanasisitiza maana kuundwa katika lugha wala si kuakisiwa. Wanaendelea kusema kuwa ishara haziwi na maana ya ndani bali huipata maana hii kupitia kwa lugha iliyohusika. Hivi ni kusema kwamba maana haifungwi kwenye ishara au mfumo wa lugha ambao ni funge.

Nadharia hii pia inaelezea kuwa ishara moja huweza kuwa na maana nyingi kwa kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii. Kwa sababu hii maana jamii inakuwa na athari kubwa juu ya maana kama tumeelezea maana ya nagona katika sehemu ya tatu ya tasnifu hii. Nadharia hii pia imejengwa katika jitihada za kubaini mbinu, nia, mikakati na vipengele vya kuichunguza na kuipata maana ya matini au kazi za kifasihi.

Nadharia nyingine itakayotuongoza katika sehemu ya nne ya kazi hii ni nadharia ya Umwingianomatini. Mkabala huu wa kihakiki unahusishwa na Julia Kristeva ambaye anaamini kuwa hamna matini yoyote ile ya fasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake. Anasisitiza kuwa lazima kuwe na matini nyingine inayohusiana nayo kwa mfano mtindo, matumizi ya sitiari, taswira, dhamira, muundo au msuko na usawiri wa wahusika. Mkabala wa mwingilianomatini unashikilia kuwa matini zina ingiliana na kuchangizana.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, kazi yoyote ile huwa na maana kwa sababu mambo fulani yanayohusiana nayo yameandikwa. Upokezi na uelewaji wa utanzu kama riwaya unategemea kuweko kwa riwaya nyingine iliyotangulia hiyo inayozungumziwa. Hata hivyo mtazamo huu haumaanishi kuwa kazi nyingine huwa zimenukuu zile zilizotangulia bali kazi hizo huchangia msimbo fulani ambao unarahisisha uashiriaji.

Tunapochunguza kazi fulani kwa mfano ***Pedro Paramo*** katika kazi yetu tunaona jinsi uashiriaji wa kazi za awali unavyosaidia katika uelewaji wa kazi za baadaye kwa hali yetu ***Nagona*** na ***Mzingile.*** Dhana hii ya mwingilianomatini inatazamwa kama jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana. Kwa sababu hii tunaweza kusema kuwa nadharia hii inachangia kile kinachoipa kazi fulani maana kama ilivyo katika nadharia iliyotangulia ya Umuundoleo.

Kwa kuzingatia mwelekeo huu tumehakiki riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** upande wa mwingilianomatini na fasihi simulizi pamoja na fasihi andishi yaani riwaya ya ***Pedro Paramo*** na ***Babu Alipokufa***. Kwa hali hii tumeona kuwa matini hufaidi kutokana na matini nyingine kama tutakavyoelezea

katika sura ya nne ya tasnifu hii. Tunapata kuwa sifa ya mwingilianomatini inajitokeza kwenye dhamira na mtindo wa kazi.

## 1:8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu umekuwa zaidi wa maktabani ambapo mbali na kusoma riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** tutazisoma kazi nyinginezo za mwandishi huyu kama vile: ***Rosa Mistika*** (1971), ***Kichwamaji*** (1974), ***Gamba la Nyoka*** (1979) na ***Dunia uwanja wa Fujo*** (1984). Tumezilinganisha kazi hizi za awali za kinathari za Kezilahabi na kuzitofautisha.

Tumetalii kazi za waandishi wengine ambazo zina mwelekeo sawa na ule wa kazi hizi kwa mfano riwaya ya ***Pedro Paramo*** (1955). ***The sisters*** (1958) ***ya D. H. Lawrence, Waiting for Godot*** (1955), ***Bina-Adamu*** (2002), ***Ziraili na Zirani*** (1979*)* na ***Babu Alipofufuka*** (2001).

# SURA YA PILI

# KAZI ZA KINATHARI ZA KEZILAHABI ZILIZOTANGULIA NAGONA NA MZINGILE

## 2:1 UTANGULIZI

Euphrase Kezilahabi ni mwandishi ambaye ameandika riwaya nyingi zikiwemo ***Rosa Mistika*** (1971), ***Kichwamaji*** (1974), ***Gamba la Nyoka*** (1979) na ***Dunia Uwanja wa Fujo*** (1981) mbali na riwaya zake ambazo ndizo kiini cha tasnifu hii yaani ***Nagona*** (1990) na ***Mzingile*** (1991).

Tumeona kuwa kuzishughulikia riwaya za awali za Kezilahabi kutatupa msingi mwema wa kuweza kuona jinsi kazi za ***Nagona*** na ***Mzingile*** zinavyohusiana na kazi za mwanzoni au jinsi zinavyotafautiana. Aidha tunanuia kuona iwapo ***Nagona*** na ***Mzingile*** zinatofautiana na kazi za Kezilahabi za Kinathari za awali na ikiwa zinatofautiana kwa kiasi gani na kwa nini hasa upande wa fani.

## 2:2 ROSA MISTIKA

Hii ni riwaya ya kwanza ya Euphrase Kezilahabi na ni riwaya ya ukuaji inayoelezea maisha ya Rosa Mistika tangu utotoni hadi utu uzima. Katika riwaya ya ***Rosa Mistika*** (1971), tunashuhudia maisha ya Rosa Mistika ambaye ndiye mhusika mkuu. Katika kazi hii suala la malezi linachukua nafasi kubwa.

Zakaria anaamini kuwa ili mabinti zake wawe salama salmini inabidi awachunge wasihusiane na wanaume. Katika kuwachunga hivi, Zakaria hatayarishi Rosa na dada zake kwa maisha yao ya ujana. Hali hii inamfanya Rosa kujitumbukiza kwa maisha ya mapenzi na kufanya mapenzi na wanaume wengi hasa anapojiunga na chuo cha walimu cha Morogoro Teachers' College. Akiwa katika chuo hiki tabia yake ya uzinzi ilienea sana hadi akapewa jina la lakabu 'Lab' (maabara) kwa sababu ya kuhusika kimapenzi na wanaume wengi. Ni wakati huu wa maisha ya Rosa ambapo Padre (wa Kikatoliki) anajaribu kumuasa Rosa bila kushughulikia tatizo lake la kimsingi; aufanyie nini uhuru ambao ameupata?

Rosa kama ua la waridi anakufa akiwa kijana na anafariki siku moja na wazazi wake. Sadifa hii ya vifo inafumbata vizuri motifu ya ufupi wa maisha. Hii ni motifu ambayo inayatawala maandishi ya Kezilahabi. Ni kama Kezilahabi anatuhimiza tutumie muda mfupi tulio nao maishani vyema hata ingawa kuna visiki vingi maishani.

Kwa upande mwingine, Regina (mamake Rosa) anaishi maisha ya kudhibitiwa na Zakaria ambaye ni mumewe ambaye daima ni mlevi. Regina anaishi maisha ya huzuni hadi kifo chake. Raha na furaha maishani na kuwepo au kutowepo kwake ni dhamira nyingine ambayo Kezilahabi anajishughulisha nayo katika kazi hii.

Riwaya hii inaelekea kukubaliana na maoni ya kidhanaishi kuwa binadamu ni kiumbe anayeteseka na anayeishi katika ulimwengu usiomjali ambao anashindwa kukabiliana nao mfano wa Rosa Mistika.

Kwa mujibu wa udhanaishi ambao ndio nadharia ambayo kazi hii ya Kezilahabi imeainishwa, binadamu kwa hali hii Rosa, anakabiliwa na tatizo kuu la uhuru. Wamitila anasema:

> *Hamna kitu cha kumsaidia katika kuutumia uhuru wake huo au kuufanya uchaguzi ambao hana budi kuufanya.* (uk.121)

## 2:3 KICHWAMAJI

Kichwamaji ambayo ni riwaya ya pili ya Kezilahabi (1974) ni hadithi ambayo matukio yake mengi yanatukia kijijini alikozaliwa mhusika mkuu Deusdedi Kazimoto.

Kazimoto anaonekana kwa mara ya kwanza katika riwaya hii akiwa nje ya ofisi ya Mkuu wa Wilaya yaani Manase. Manase anabagua wazee kwa kuhudumia wasichana ambao ni marafiki zake. Anamfukuza mzee kutoka ofisini mwake kwa madai ya kosa la kuingia ofisini mwake akiwa amebeba fimbo.

Hali hii imesababishwa na mkengeuko ambao umetokana na mfumo wa kielimu wa kikoloni na vile Waafrika waliosoma wameshikilia mienendo ya kimagharibi.
Ukengeushi huu unaojitokeza pia unahusishwa kwa kiwango kikubwa na mazingira ya mjini, ubinafsi wa mwanadamu na kujielewa kwake.

Kazimoto naye anazikosa huduma za Mkuu wa Wilaya (Manase) kwa kuwa upo ugomvi baina yao wa Manase kumtunga mimba Rukia ambaye ni dadake Kazimoto. Aidha kuna kutoelewana baina ya familia zao ambapo

Mafuru babake Kazimoto anahamishwa na serikali kutoka kwa shamba ambalo lilikuwa mali ya Kabenga babake Manase. Tukio hili linamfanya Kazimoto kulipiza kisasi kwa kuchoma nyumba ya Kabenga. Aidha anafanya urafiki na Vumilia ambaye inasemekana kuwa ni rafikiye Kabenga.

Hali hizi huchora taswira ya ukosefu wa maana katika maisha. Maisha yamejaa misukosuko, wivu, kisasi na ukosefu wa utu kwa kiwango kikubwa hata sehemu za

vijijini hazikuachwa nyuma. Baadaye, Kazimoto anamchumbia na kumwoa Sabina ambaye ni dadake Manase. Ndoa hii inaelekea kuunga familia hizi ambazo hapo awali zilikosa kuelewana.

Sabina anapata mimba na kuzaa njiti (mtoto ambaye ni mfu) Kwa upande mwingine Manase naye anapata mtoto ambaye anazaliwa akiwa na kichwa kikubwa ambacho kimetokana na ugonjwa wa zinaa ambao pia kisadfa; ndio ulioua mtoto wa Kazimoto.Hata daktari anayeutibu ugonjwa huu anafariki. Hii ni ishara ambayo inaelezea mateso yanayompata binadamu katika uchaguzi wowote anaoufanya.

Kazimoto anapogundua hivi, anaamua kujiua. Anafikiri kuwa alisababisha kifo cha kakake Kalia kwa kumpa mwelekeo mbaya wa maisha. Ni dhahiri kuwa wahusika hawa wawili wakuu Manase na Kazimoto hawauthamini utamaduni wa Kiafrika. Manase anaudharau muziki wa Kiafrika ambao anasema kuwa unalia mbu! mbu! mbu! Tangu mwanzo hadi mwisho anausifu muziki wa kizungu. Hizi ni ishara kubwa za mkengeuko kwa

mhusika huyu ambao umesababishwa na elimu ya kizungu. Mkengeuko ni sifa muhimu ya udhanaishi. Kwa kiasi kikubwa riwaya hii imeghushi falsafa ya udhanaishi kuliko labda kazi yoyote nyingine ya Kezilahabi.
Fikra hizi ni mwangwi wa mhusika mkuu Ramatoulaye katika ***"God's Bit's of Wood"*** ambaye pia amesoma elimu ya kikoloni. Anaona aibu kubwa kuhusu watu wake na utamaduni wake. Mbilikimo wa Kiafrika wanapoonyeshwa katika sinema anakana kuwa hao ni Waafrika halisi. Wakati mwingine anapotazama sinema, anawakemea watu wanaozungumza nyuma ya pale alipoketi huku akiwaita wajinga kwa lugha ya Kifaranza. Huu ndio mkengeuko uletwao na elimu ya kikoloni.

Ufupi wa maisha unajitokeza kwa riwaya hii kupitia kwa taswira ya makazi ya Manase. Mabaki ya lililokuwa gari la familia ni makazi ya ndege sawia na taswira ya Pate baada ya maanguko ambapo bundi walifanya makazi katika magofu ya nyumba za wafalme katika ***Al -Inkishafi***

Aidha swala la kifo limeshughulikiwa sambamba na maana ya maisha. Maisha ni kama kifo cha polepole. Manase anasema

*Tunapoishi tunakufa, kwa hiyo Kufa ni kuishi* (uk. 206)

Mpaka baina ya kifo na uhai unaelekea kuwa mwembamba sana. Mwelekeo wa kazi hii vile vile ni wa kidhanaishi ambapo ufupi wa uhai unasisitizwa pamoja na ukengeushi. Katika ***Kichwamaji*** Kezilahabi ameyaangalia masuala yanayohusiana na maisha, maana yake au kutokuwepo kwa maana hiyo; nafasi ya mtu binafsi katika jamii na furaha ya mwanadamu katika maisha yake.

## 2:4 DUNIA UWANJA WA FUJO

Katika riwaya ya ***Dunia Uwanja wa Fujo***, Kezilahabi ametumia taswira ya fujo kuelezea hali ya maisha ya binadamu. Tofuati na riwaya iliyotangulia riwaya hii inamulika zaidi suala la furaha katika maisha ya mhusika.

Ili kuelezea taswira hii, mwandishi anamtumia mhusika Tumaini. Wazazi wa Tumaini wanafariki na kumwachia urithi wa shilingi elfu hamsini ambazo kwa wakati huo zilikuwa pesa nyingi. Hata hivyo, Tumaini anaamua kuacha shule na kuanza maisha ya ureda. Suala la malezi kumwathiri mhusika linatokea tena kama vile lilivyotokea katika ***Rosa Mistika.***

Hatimaye anahama kijiji cha Bugolola baada ya vitendo vyake kuwakasirisha wanakijiji. Anahamia mjini Mwanza kisha baadaye anahamia Shinyanga kwa

kukosa kuridhika na raha za mji wa Mwanza.Tumaini akiwa Shinyanga, anaendelea na maisha ya ureda hadi pesa zote alizorithi zinaisha.
Tumaini analazimika kutafuta kazi kwa Dennis (mkuu wa upelelezi mkoani) ambaye anamfanyia mpango na kumpa kazi ya upelelezi. Hapa, Tumaini hapati furaha na utulivu kwa kuwa anafanyiwa njama na mwenye African's Royal Bar ambaye anaona kuwa Tumaini apeleleza bar yake. Mama Resi ambaye anaona kuwa Tumaini anampoteza mumewe na pia hapendezwi na umaarufu wa Tumaini na Makoroboi. Makoroboi ni jambazi ambalo linamwomba Tumaini asiwaambie wanakijiji kuwa yeye ni mwizi lakini Tumaini anaitoboa siri yake. Hawa (mama Resi na Makoroboi) wanaingia

kwenye mipango ya kumwangamiza Tumaini. Baadaye Tumaini anapigwa vibaya hadi anaamua kujiuzulu na kuanza kilimo cha pamba.

Kazi ya kilimo inamwendea vizuri hata anaajiri watu kumfanyia kazi. Anafaulu kujinunulia gari.Akiwa mbioni kujilimbikizia mali, tangazo la azimio la Arusha linatokea linalowataka watu kuhamia vijiji vya ujamaa kufanya kazi pamoja.

Mambo haya hayampigi mshipa Tumaini hadi pale hadhara ya watu inapomwita mnyang'anyi na serikali kutwaa shamba lake. Kama njia ya kulipisha kisasi, Tumaini anamuua Mkuu wa Mkoa naye anapigwa risasi mguuni na polisi na baada ya kupona anapelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifo.

Katika riwaya hii tunaona jinsi ambavyo mwandishi anajishughulisha na masuala ya kidhanaishi kama vile maana ya maisha,dhana ya uteuzi, dhana ya Mungu na furaha. Maisha katika riwaya hii yamejaa fujo, si kijijini si mjini. Hata Tumaini anapouhama mji mmoja kwa matarajio ya kupata nafuu kwa mji mwingine, fujo zinamwandama huko. Dunia yote kweli ni uwanja wa fujo kulingana na riwaya hii.
Bidii anazotia Tumaini (binadamu) katika kujitoa kwa fujo ya dunia hazifui dafu.

Falsafa hii kuhusu maisha ambayo Kezilahabi anaishughulikia imejikita katika hali halisi ya kihistoria. Hii ni Tanzania baada ya Azimio la Arusha.Azimio la Arusha lilipinga unyonyaji na kuhimiza Watanzania

kujitegemea. Hali hii inalazimu mali ya Tumaini kutwaliwa kwa kuwa anawakilisha unyonyaji uliopingwa na Ujamaa.

Mabadiliko haya yanazua mgogoro mkubwa katika maisha ya Tumaini ambaye tunaweza kusema kuwa ni kiwakilishi cha upinzani dhidi ya sera za ujamaa na kushindwa kwake kunamaanisha kuwa siasa ya ujamaa ilifaulu. Aidha suala la nafasi ya mtu binafsi dhidi ya jamii linajitokeza vizuri katika riwaya hii hasa tunapoangalia hatima ya Tumaini ambaye anauliwa mbele ya bendera ya taifa. Hii ni ishara kuwa taifa ni muhimu kuliko mtu binafsi.

Ni muhimu kusema kuwa Kezilahabi anakuza na kuendeleza falsafa yake kuhusu maisha kihatua katika riwaya zake.

## 2:5 GAMBA LA NYOKA

Katika riwaya ya ***Gamba la Nyoka***, Kezilahabi ameshughulikia utekelezaji wa sera za Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa kwa kina zaidi kuliko alivyofanya katika ***Dunia Uwanja wa Fujo***. Aidha anaonyesha jinsi utekelezaji wa Azimio la Arusha ulivyojaa dhuluma na ufisadi mtupu. Katika riwaya hii, Kezilahabi anaichora picha ya hali hii tunaposhuhudia vile wanakijiji wa Bucho wanatumiwa kuwahamisha wanakijiji wa Kisole wanavumilia jua kali wakisikiliza hotuba ya Mkuu wa Wilaya ambayo inadhamiriwa kuwa funzo kuhusu siasa.

Baadaye wanakijiji hawa wanahamishwa wakati mvua nyingi inanyesha. Taswira hizi zinaonyesha vile ambavyo sera za siasa ya Ujamaa zilivyotekelezwa vibaya. Aidha Mamboleo na Mambosasa ambao ni

viwakilishi wa viongozi wapotovu wametumiwa kubeza sera hizi. Mamboleo anasema:

> *Lakini watu hawakuanzisha wazo la*
> *ujamaa. Wazo hili limetoka juu na*
> *kuwaangukia watu kama jiwe walibebe.*(uk.51)

Ni dhahiri basi kuwa wananchi hawakuchangia sera hizi bali sera zilizolazimishwa kwa nguvu zilizowazidi.

Mbali na siasa ya Ujamaa, katika ***Gamba la Nyoka*** Kezilahabi ameshughulikia unafiki wa kidini na upofu wa wafuasi wa kidini kupitia kwa Padri Mandevu na mfuasi wake mmoja Mama Tinda. Mama Tinda anaikubali dini pamoja na kila anachotaka Padri Mandevu huku akidhania kuwa hilo ni jukumu lake kama mfuasi mwema wa Mungu hali ambayo inaelekea kulingana na tashtiti iliyopo katika tamthilia ya ***Masaibu Ya Ndugu Jero*** ambapo Chume anakubali kumpiga mkewe (Amope) anaposhauriwa kufanya hivyo na ndugu Jero ( Mtu wa Mungu kwa maoni ya Chume).

Mbali na kubeza unafiki katika dini mwandishi anaonyesha kuwa siasa ya Ujamaa ilishindwa kwa sababu ya udhaifu wa viongozi na matatizo ya utendaji ya Azimio la Arusha. Ingawa ukoloni ulichangia katika kushindwa kwa ujamaa, viongozi waliounzisha wanalaumika kwa sababu hawakufanya maandalizi ya kutosha na pia walijaribu kutumia njia ya mkato na kufanya mambo kwa pupa ili kuleta mabadiliko ya kijamii. Matokeo ya udhaifu huu yakawa maangamizi makubwa ya watu wa kawaida tunayoyaona katika ***Gamba la Nyoka*** .

Riwaya nyingine zinazoshughulikia suala la utekelezaji wa sera ya ujamaa na udhaifu ulioandamana na utekelezaji huo ni kama: ***Nyota ya Huzuni*** (1980), ***Njozi Iliyopotea*** (1980 ). Riwaya hizi zinaonyesha kuwa mbali na dhuluma zilizodhihirika katika utekelezaji wa sera ya ujamaa, ufisadi nao ulichukuwa sehemu kubwa na kuifanya vigumu kuelewa undugu uliokuwepo katika huu ujamaa. Hali hii inatokea katika riwaya ya ***Njozi Iliyopotea*** katika wasifu wa Lupituko (katibu wa chama) ambaye anapowazungumzia watu hawaonyeshi heshima yoyote hasa wazee. Anaona kuwa mamlaka yamemweka katika ngazi ambapo anawabeza watu bila kujali bora anaelekeza azimio la ujamaa.

## 2:6 HITIMISHO

Tunapoziangalia riwaya za Kezilahabi zinazotangulia ***Nagona*** na ***Mzingile*** tunaona kuwa masuala ya kifalsafa yameshughulikiwa yakiwemo maana na thamani ya maisha, dini na mahala pake katika jamii na hata kifo. Haya ni masuala ya kidhanaishi lakini katika hali halisi ya Tanzania tangu Uhuru hadi wakati baada ya Azimio la Arusha.

Hii ni mojawapo ya sababu kuu ambayo inaifanya kazi za awali za Kezilahabi za kinathari kutofautiana na ***Nagona*** na ***Mzingile.*** Kazi hizi za awali zimekitwa zaidi katika hali halisi yaani mandhari ni ya kihistoria. Suala hili la uhalisi pia linaathiri usawiri wa wahusika tofauti na ***Nagona*** na ***Mzingile*** ambapo mandhari yake hayakitwi kwenye uhalisia na mwandishi anawatumia wahusika batili.

Kinachojitokeza wazi katika *Nagona* na *Mzingile* ni kuwa masuala haya ya kifalsafa yamejadiliwa na mwandishi lakini kwa mwelekeo tofauti na ule wa kazi zake za awali za kinathari. Hivi ni kumaanisha kuwa kazi za Kezilahabi za awali za kinathari zinahifadhi na kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi kama vile wahusika ambao sifa zao ni za watu wanaopatikana katika jamii halisi, usawiri wa mazingira ya kawaida kama vile Tanzania kabla na baada ya uhuru na hata usimulizi unaokisi hali inayokaribiana na ulimwengu halisi.Hali hizi ni tofauti na *Nagona* na *Mzingile* kama tumejadili hapo juu.

# SURA YA TATU

# SITIARI NA JAZANDA KATIKA NAGONA NA MZINGILE.

## 3:1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulikia baadhi ya sitiari na jazanda zilizotumika katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** ili kukuza ujumbe ulio katika riwaya hizi.
Hivi ni kusema kuwa katika kuzielezea sitiari na jazanda hizi ni lazima vilevile turejelee baadhi ya maudhui ya kazi hizi za Kezilahabi kama nadharia ya Umuundoleo inavyoelezea kuwa maana huundwa katika lugha.
Kulingana na Wamitila:

> *Sitiari ni tamathali ya usemi ielezeayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Kwa hali hii tunaweza kusema kuwa sitiari imejengeka katika uhamishi wa maana* (uk. 202).

Aidha Wamitila anaelezea kuwa matumizi ya sitiari hulenga hisia au fahiwa fulani au kujenga picha au taswira fulani. Mbatiah naye ana maoni yayo hayo kuwa sitiari hutumia ulinganishi na uhamisho wa maana. Kinachodhihirika hapa ni kuwa sitiari zinahusu uhamishi wa maana na uhamishi huu huchangia maana ya kazi hasa katika fasihi.

Matumizi ya sitiari yamefungamana na matumizi ya jazanda ambazo hutumia picha kuelezea hali au kitu na hukuzwa kutokana na maelezo au tamathali za usemi kama tashbihi Sitiari na jazanda zinachangia kukuza na kujenga maudhui katika ***Nagona*** na ***Mzingile.***

Cuddon anaelezea jukumu la sitiari na jazanda kuwa:

> *Sitiari huweza kuelezea na kufafanua dhana, vitu, watu, hisia na hali mbalimbali* (uk. 186).

Katika sura hii tutazitalii sitiari na jazanda alizotumia Kezilahabi na jinsi ambavyo zimetumika kufafanua maudhui ya kazi hizi mbili. Mwandishi ametumia lugha kama nyenzo ya kuelezea ulimwengu. Hivyo tunategemea sitiari kuuelezea ulimwengu na hali hii inafumbata vizuri nadharia ya Umuundoleo inayotilia mkazo dhana ya maana kuundwa katika lugha.

### 3:2 *NAGONA* NA *MZINGILE*

Katika ***Nagona*** tunamkuta msimulizi akiwa safarini na tayari yu katikati ya kijiji. Msimulizi huyu anaonekana kutokuwa na hakika iwapo huu ulikuwa mwanzo wa safari au sio. Baadaye tunagundua kuwa hii si safari ya kawaida bali ni safari ya kisitiari kwa kuwa babu yake msimulizi anasema:

> *Usiwe na haraka kuna vikwazo vingi, lakini kushinda vikwazo si kuufikia ukweli. Safari ni ndefu, lakini kusafiri si kufika. Jambo muhimu ni kufikiri* (uk.24).

Maneno haya ya babu ni muhimu sana kwa kuwa yanatuelezea mambo ya kimsingi katika ***Nagona*** na ***Mzingile.*** Kwanza kabisa ni kuwa safari anayoifanya msimulizi ina lengo la kuufikia ukweli hivyo si safari ya kawaida bali ya kifikra. Pili, kwamba ukweli wenyewe unakabiliwa na vikwazo vingi mtu/binadamu anapojaribu kuutafuta na haimaanishi kuwa ukweli wenyewe utafikiwa.

Kwa kiwango kikubwa haya ndiyo masuala anayoyafumbata Kezilahabi kwa mtindo wa sitiari na jazanda. Kazi hizi mbili zimejaa sitiari ambazo tutaelezea katika sehemu zinazofuata za kazi hii. Nadharia ya Umuundoleo ambayo ndiyo kiunzi cha tasnifu hii inasisitiza kuwa lugha huchukua nafasi kubwa katika kuuhakiki na kuuchanganua mpangilio na maana ya kazi fulani. Hivyo maana huundwa katika lugha na hivi ndivyo ilivyo katika ***Nagona*** na ***Mzingile***. Ndiposa tutashughulikia nafasi ya sitiari na jazanda katika kazi hizi.

Kwanza kabisa, tutaelezea maana ya taswira ya safari ambayo kwa kazi hizi inawakilisha maisha ya binadamu yalivyo.Katika ***Nagona***, msimulizi katika safari anapitia mandhari ya kiajabu, msitu unamcheka, anapigwa viboko bila kuona anayempiga, anaingia kwa nyumba ambamo milango inajifunga na kujifungua. Taswira hizi zote zinaelezea lile onyo alilotolewa msimulizi na babu yake kuwa safari ambayo kwa hali hii ni maisha ya mwanadamu na juhudi zake za kuusaka ukweli ina vikwazo vingi. Vingine miongoni mwao vinaweza hata kumithilishwa na vioja kama hivi anavyokumbana navyo msimulizi katika ***Nagona.***

Si maajabu tu ambayo ni vikwazo, safari au maisha yanampeleka katika mazingira ya bonde lenye giza, msitu, ukungu na maluweluwe. Hali kama hizi zinadhihirisha hali ya kutatiza na kutojua kunakompata binadamu akiwa mbioni kuusaka ukweli. Mtu anapokuwa gizani haoni mbele. Akiwa msituni wanyama wa mwitu humtisha na hata njia inaweza kuwa ngumu kuipata. Taswira hizi zinazoakisi ugumu wa juhudi za kuutafuta ukweli zinazidi kuongezeka kwa jinsi ambavyo maisha (safari) yanavyoendelea.

Katika sura ya tano, msimulizi anajikuta msituni ambapo mwanamke anamhimiza achukue upinde na mshale na amwinde paa hadi amshike mkononi na kumjua. Paa hapa ametumika kiisitiari kuuashiria ukweli na maarifa. Paa kwa kawaida ni mnyama mwepesi na mwenye mbio. Inambidi msasi anayemwinda amfuate kwa mbio na kutumia maarifa ili kumpata. Hali hii ya ugumu wa kuyapata maarifa na ukweli ndiyo inayoelezwa kwa kutumia sitiari ya paa. Katika msako wa kumtafuta paa, msimulizi hakuweza kuziona nyayo za paa aliyekuwa anamwinda mara nyingi katika msako huo.

Katika safari yake msimulizi anakutana na Nabii na Mtume ambao wanajitolea kufuatana naye ili wamsake paa (ukweli) pamoja. Hali hii inaashiria kuwa juhudi za kuutafuta ukweli si jukumu la mtu mmoja. Mtume na Nabii hapa wanasimamia Uislamu na Ukristo. Dini hizi zimekuwa mbioni kuutafuta ukweli kwa karne nyingi. Baadaye msimulizi anakutana na Mtenzi na Mfuasi ambao wanafuatana naye katika safari hii. Wanapitia mlima mrefu ambapo nyayo za paa zilikuwa zikipotea. Mtume alifanikiwa kuuhamisha mlima (kukiondoa kikwazo hiki) na wakafanikiwa kuziona nyayo za paa (ishara ya ukweli), lakini kizuizi kingine kilikuwa kikiwasubiri kwa kuwa walifika nyikani mwenye majani marefu na hapa walipoteza zile nyayo za paa tena lakini wakaongozwa na Mfuasi ambaye alielekea kujua njia aliyoifuata paa.

Hata hivyo vizuizi hivi viliongezeka tena walipofika bondeni. Bonde lilikuwa na mto na hapa nyayo za paa zilipotea tena. Taswira hizi zote (bonde, mlima, nyika na mto) zinadhihirisha vile juhudi za kuusaka ukweli zinavyokabiliwa na vikwazo vingi.

Katika ***Mzingile*** vilevile kuna taswira kama hizi zinazoakisi ugumu wa kuutafuta ukweli na maana ya maisha. Katika riwaya hii, msimulizi alikuwa ametumwa kupeleka tanzia ya kifo kwa mzee (babake marehemu); ambaye pia ametumika kama ishara ya Kristo au Mungu. Safari hii ya kutafuta maana ya maisha inampeleka msimulizi kwa milima na mabonde. Msimulizi anasema:

> *Haikuwa rahisi kupanda na kuvuka milima hiyo iliyojulikana katika historia na iliyoficha kilichokuwa upande wa pili* (uk.6).

Msimulizi katika ***Mzingile*** anaelezea kuwa alipovuka milima, alifika mahali palipokuwa na njia tatu na mojawapo ya njia hizi ilikuwa imezibwa kwa miba na nyuma ya njia hii ndiko kulikuwa na njia wazi. Hata alipoweza kuiondoa miba na kumfuata ndege ambaye kwa matamanio yake angempa mwongozo, anamfikia mwanamke ambaye anadhania atamwongoza njia ambapo wanafika jangwani penye mchanga mwingi na msimulizi kama anavyosema hakuwa na ufundi wa kutembea mchangani-hivyo mchanga ulizirudisha hatua zake nyuma.

Taswira hizi (mlima, njia panda, miba na mchanga) pia zinaakisi ugumu wa kutafuta ukweli na maana ya maisha na vizuizi vinavyotokea binadamu anapotia bidii kuutafuta huu ukweli na maana ya maisha. Taswira hizi zinaelezea mwelekeo wa usasaleo kuhusu maisha kama anavyoelezea Wamitila:

> *Ukweli unatazamwa kama kitu kisichoweza kufikika ni kama binadamu huwa katika harakati kubwa za kujaribu kuufikia* (uk.126).

Sitiari na taswira zinazotumika katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** hazionyeshi ugumu wa kuusaka ukweli na maana ya maisha pekee bali zinaonyesha picha ya jinsi ambavyo binadamu wengine huwa vikwazo katika jitihada hizi. Katika ***Nagona*** tunaelezwa kuhusu wale walioaminika kuongoza watu katika njia ya kweli na msimulizi anatoa mifano wa Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud na Nietzsche.

Msimulizi anasema:

> *Hiki ni kikundi kidogo tu cha wale walioiwekea njia miba, ngazi za kupandia na madaraja yasiyoaminika. Walijaribu kuiondoa miba, ngazi na madaraja yaliyowekwa na wale waliotangulia lakini kwa kufanya hivyo waliweka vikwazo vingine badala yake (uk.15).*

Hawa waliaminika kuwa wangerahisisha juhudi za kuutafuta ukweli lakini badala yake walizitatiza juhudi hizi kwa kuongezea vizuizi. Taswira hii ya kuweka ngazi na madaraja yasiyoaminika inaweza kuelezwa kwa njia mbili. Kwanza kabisa, kuwa wanafalsafa waliotangulia kuelezea kuhusu maisha walitia juhudi mbalimbali kuufichua ukweli lakini wakawa wametumia njia (madaraja na ngazi) ambazo hatimaye zilielekea kuwa vikwazo kwa vizazi vilivyowafuata. Hivyo tunapata kuwa mikabala ya wataalamu hawa ya kuyaelewa maisha, kuufasiri ukweli na kuichambua hali halisi ya binadamu ilikuwa tofauti kwa mfano baadhi yao kama Socrates walikuwa na mwelekeo wa kifalsafa, Darwin, mwelekeo wa kibiolojia na Nietzche wake ulikuwa wa kidhanaishi.Katika ***Nagona*** tunaambiwa:

> *Wote waliimba nyimbo nyingi za ngoma lakini hawakuweza kukaa katikati ya duara mwanga ulipotokea; kitovu kikapasuka, pakabakia shimo ambamo kizaki kilichofuata*
> *kilitumbukia* (uk.15).

*pakabakia shimo ambamo kizaki kilichofuata kilitumbukia* (uk.15)

Maelezo haya yanaelezea kuwa mwongozo waliotarajia kuutoa kwa vizazi vya baadaye ulileta mkinzano badala ya kuuweka ukweli wazi.

Tukiiangalia taswira hii kwa mtazamo mwingine tunaweza kuulinganisha na hali ya kushikilia na kung'ang'ania kaida za utunzi au uandishi wa kazi kuwa ndizo tu zinazofanya kazi kuwa kubalifu. Kwa mfano kwa muda mrefu baadhi ya watunzi wa kazi za kifasihi walikuwa wameshikilia kuwa riwaya inahitaji kufuata kaida fulani za utunzi kama vile msuko na visababishi vyake.

Mfano kama huu unaonyesha hali za kitaswira za kuziwekea njia miba ambayo lazima iondolewe ndipo njia iweze kuwa wazi na kupitika. Kwa kutumia mfano huu hatusemi kuwa mwelekeo wa tapo la uhalisia wa kijadi ulikuwa haufai bali tunasema kuwa hii si njia ya kipekee ya kujielezea katika fasihi. Tunachosema ni kuwa kuna namna nyingi ambazo kupitia kwazo mawazo na kazi zinaweza kuandikiwa na zikaweza kuwa na maana kamili kama nadharia ya Umuundoleo inavyosisitiza.

Kwa mtazamo huu riwaya hizi zinaelekea kuidadisi miundo na mikabala ya uandishi katika fasihi ya Kiswahili na kuishia kuwa aina ya 'meta-riwaya' (riwaya inayotoa kauli au maoni kuhusu riwaya)

Kezilahabi pia ametumia taswira ya Padri mlevi kuonyesha jinsi dini za Kikristo na Kiislamu zilivyoshindwa kutatua masuala muhimu kuhusu maisha. Katika ***Mzingile***, Kezilahabi anachora taswira ya Padri aliyekuwa

anaomba ili ukame umalizike lakini haukuisha na katika kata tamaa yake, alianza kushiriki ulevi kwa kuchanganya pombe za kwao na za kienyeji. Msimulizi anasema:

> *Katika ulevi wake alivunjavunja masanamu kanisani. Alisikika akipiga kelele. "Mungu gani wewe! Umeniaibisha mbele ya watu weusi* (uk.20).

Kezilahabi anaelezea kuwa binadamu huwa mbioni kuutafuta ukweli kanisani kwa jumla na hiki ndicho kitendawili katika jazanda hii maana mwanadamu anaonekana kulewa dini badala ya kuupata ukweli kama Marx alivyosema kuwa dini ni bhangi ya akili. Aidha kitendo cha padre kuchanganya pombe za kwao na za kienyeji kinaweza kuonyesha umahuluti unaoonekana katika ulimwengu wa leo ambapo mipaka ya kitaifa, kidini, kilugha kiitikadi na ki-mtazamo inaelekea kufutwa.

Hali hii ya kushindwa kuupata ukweli katika dini imeelezewa kiistiara na D H. Lawrence katika ***The sisters*** ambapo Padri pia anachorwa kama kiongozi aliyekosa kuidhibiti kazi yake kwa kuwa "makono yake" makubwa yalikuwa yakitetemeka kiwango cha kuwa hangeweza kushikilia kisanduku chake chenye ugoro ili atie tumbako hiyo puani.
Taswira hii bado inaelezea kuwa ugoro mara kwa mara uliharibu na kutia weusi joho lake la Kipadri. Sitiari hii inaweza kufasiriwa kuakisi kushindwa kwa dini kutatua matatizo na kuelezea masuala ya maisha ya binadamu (Padri).

Sitiari nyingine katika kazi hizi zinaelezea hali inayosababisha ugumu wa kuufikia ukweli. Katika ***Mzingile***, Kezilahabi ametumia sitiari ya sayari

kuelezea maisha ya binadamu yalivyo. Msimulizi katika ***Nagona*** anasema kuwa dunia katika mwendo wa kulizunguka jua inajiviringisha yenyewe kwenye mhimili wake hali ambayo anafananisha na binadamu kuwa ana mhimili wake mwenyewe ambapo anajiviringisha akiwa mbioni kulizunguka jua lake lisiloonekana.

Tofauti iliyopo katika kifananishi hiki ni kuwa dunia inapozunguka jua, tunapata mabadiliko ya mchana na usiku lakini binadamu anazunguka jua lake lisiloonekana tunaweza kuifasiri hali hii kuwa ina maana mbili. Kwanza kabisa ni kuwa binadamu anazunguka kitu kisichokuwepo.
Huu ni mwelekeo ulio sawa na ule wa kidhanaishi na kiubwege kuwa maisha yana utupu hali ambayo inaelekea kulingana na ile ya wahusika wa ***"Waiting for Godot",*** ambao wanamsubiri Godot ingawa hawajui atakuja lini. Pili, mwendo wa sayari ni wa kujirudia. Katika sitiari hii binadamu anatia juhudi kubadilisha hali yake kwa kulizunguka jua lake lakini anashinda mahali pale pale na jua lake ambalo lina mwanga wa kubadilisha hali hii halionekani.

Hali hii ya kutapatapa kwa mwanadamu bila kuupata ukweli inatiliwa nguvu na taswira ya viongozi wa kisiasa ambao wanaongoza watu katika vichochoro vya kiuchumi vilivyoachwa kutumika zamani. Hii taswira ya vichochoro vya kiuchumi inaelezea vile mataifa ya ulimwengu wa tatu yanavyozidi kubaki nyuma hasa kuhusu masuala ya kiuchumi. Tunabaki tukifanyia majaribio mambo ambayo mataifa mengine hasa ya Ulaya yamekwishayapitia. Matokeo ya kupitia vichochoro hivi ni kuendelea kubaki nyuma kiuchumi huku tukiililia misaada kutoka kwa wafadhili.

Kwa kiasi fulani Kezilahabi anaiendeleza dhamira hii katika tamthilia yake ya ***Kaptula ya Marx,*** ambapo rais Kapera analiongoza baraza lake kwenye safari ya kimzunguko kuutafuta usawa na ukweli

Taswira hii ya vichochoro vya kiuchumi inatiliwa uzito na sitiari ile ya wataalamu kuacha jahazi liendeshwe na upepo. Msimulizi katika ***Nagona*** anasema kuwa katika kuyumbayumba waligonga mwamba.... penye ufa pakazibwa na pamba. Sitiari hii inaonyesha vile matatizo ya nchi changa yanavyotafutiwa suluhu zisizo za kudumu kwa hali hii, ufa unaozibwa kwa pamba hata maji yakija kwa mkondo mwepesi kiasi gani, bado yatapenya ule mwanya na kupita na ile pamba iliyotumika kuuziba ule mwanya.

Hali hii inaonyesha kuwa si wanafalsafa tu ambao hawajaweza kutoa mwelekeo wa kupata ukweli hata wanasiasa hushinda wakitolea nchi zao suluhu za muda mfupi (kuziba ufa kwenye jahazi kwa pamba).

Hii mifano inaonyesha kushindwa kwa asasi ambazo mwanadamu ameziweka ili kuutafuta ukweli. Hivyo ni kama mwandishi anatupendekezea kuwa juhudi za kuutafuta ukweli zinahitaji bidii kubwa na kila sekta ya maisha kuhusika. Hii ndiyo sababu msimulizi katika ***Nagona*** anamfuata paa na wasaidizi wake, wanayapitia majaribu makubwa kabla ya kumfikia paa (ukweli) na hata baada ya kumfikia paa huyu bado anamkwepa kumaanisha kuwa ukweli huo pia unamkwepa.

Kilele cha ushinde huu ni ile taswira ya ngoma kuu ambayo ni siku ambayo makundi mbalimbali yalitarajiwa kushiriki kutoa mwongozo kuhusu maisha.

Siku hii ilishirikisha mwanafalsafa, wanasaikolojia, wanamapinduzi na watu wote ambao walicheza ngoma zao kwa zamu katika duara.

Katika duara hii, sehemu ya kati ilikuwa na mwanga ambao pia ni sitiari ya ukweli. Baada ya makundi haya kushiriki ngoma hii iliyojaa vurumai, makundi yote yalitulia yakiutazama mwanga uliokuwa umeshuka kutoka juu. Hata hivyo msimulizi katika Nagona anasema:

> *Nilipotazama juu niliona mwanga ukipanda juu na kuacha giza kwetu.*
>
> *Sote sasa tulipiga kelele tukitazama juu, "nagona! nagona!" Polepole mwanga ulipanda juu ukatoweka kabisa, tukabaki gizani.*

Hizi sitiari za mwanga na nagona zinaonyesha kuwa makundi haya yaliyoshiriki katika ngoma kuu yalitarajiwa kutoa mwongozo wa kupata ukweli kwa kutumia mbinu zao tofauti tofauti lakini hayakufua dafu na hatimaye ukweli (mwanga) ulitoweka na kuwaacha wote katika giza (kutojua).

Hii sitiari inaelezea juhudi za miaka mingi za makundi ya wataalamu mbalimbali za kuutafuta ukweli ambao hawajafanikiwa kuupata. Ulimwengu umebaki kuwa kama uwanja wa fujo vile Kezilahabi anavyouchora katika ***Dunia uwanja wa fujo.*** Hata tunaweza kukubaliana na sitiari anayoitumia mwanamke katika ***Nagona*** anapoiita dunia tambara bovu ambapo ni vigumu kupaishi.

### 3:3 SITIARI ZINAZOUAKISI UKWELI

Kezilahabi ameelezea katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** vile maisha yalivyo kwa kutumia taswira ya safari na vile ambavyo binadamu hutia juhudi kutafuta ukweli maarifa na hata maana ya maisha yake lakini mbio hizi za kuusaka ukweli, aidha hukumbwa na matatizo si haba.

Katika sehemu hii tutaelezea baadhi ya sitiari zinazosimamia ukweli katika kazi hizi mbili. Mojawapo ya sitiari zinazowakilisha ukweli ni ile ya paa. Paa kama nilivyoelezea katika sehemu iliyotangulia ni mnyama mwepesi na anahitaji kuwindwa na msasi mwenye juhudi na maarifa ili apatikane. Paa huyu anayetafutwa na msimulizi, anatakikana amshike mkononi amjue katika safari hii. Paa mwenyewe anayewindwa mwanzoni haonekani ila ni nyayo zake tu zinazoonekana.

Nyayo hapa ni dalili za ukweli ule. Mara nyingi binadamu anapoutafuta ukweli iwe ni kwenye maabara au vitabuni, mwanzoni ni dalili tu zinazoonekana. Daktari anayefanya uchunguzi wa ugonjwa katika maabara huwa hauoni ugonjwa ila viini tu au virusi vya ugonjwa ambavyo ni dalili tu za ugonjwa ule. Hii ndiyo maana inayofumbatwa na ugumu wa kumpata paa kwa kuwa ni nyayo zake tu zinazoonekana.

Msimulizi katika ***Nagona*** anapitia mandhari yanayotatiza katika juhudi zake za kuutafuta ukweli (paa). Anapitia mazingira ambayo yamejaa giza, maluweluwe na ukungu hali ambazo zinafanya juhudi zake za kuziona nyayo (dalili) za huyu paa (ukweli) ngumu sana. Inabidi msimulizi afuatane na wasaidizi wengine (Nabii, Mtume, Mtenzi na Mfuasi ambao kila mmoja wao ana maarifa tofauti ili waweze kumfikia paa (kweli).

majaribu mengi kama vile kuilima ardhi ngumu, kuuhamisha mlima, kumletea mfalme kiko na hata kucheza bao na paa na kumshinda ndipo wampate.
Majaribu haya yote yanaonyesha kuwa juhudi za kuupata ukweli zinahitaji maarifa tofauti tofauti na kuwa hata yanapotumika, ukweli bado una njia ya kumkwepa binadamu. Katika msako huu msimulizi anafaulu kumpata paa lakini wanaporudi naye, hapati nafasi ya kumkaribia na kumshika.

Hatimaye paa ambaye sasa ni mwanamke mrembo anampiga mieleka na kumshinda msimulizi na kutoweka. Ukweli ambao alidhania ameutia mkononi na kuuenzi ulimkurupuka na kumwacha. Hivi ni kumaanisha kuwa ukweli una utelezi mwingi labda Kezilahabi anatuomya dhidi ya kujigamba kuhusu maarifa tuyapatayo kuwa yana utelezi. Mwanamke katika ***Nagona*** aliyecheza mieleka na msimulizi alikuwa hashikiki kwa kuwa alikuwa na utelezi mwingi. Aidha tunaweza kusema kuwa mwanamke ni ishara ya uzawa. Anafumbata kiishara kanuni ya usanii. Kwa hali hii tunapata kuwa mwandishi ameweza kutumia lugha kuleta maana mbalimbali kama nadharia ya umuundoleo inavyoelezea.

Sitiari nyingine inayoeleza ukweli na sifa zake ni sitiari ya ***Nagona***. Katika mjadala wa msimulizi na babu yake, babu anamwambia:

> *Kwa muda wote wa uhai wangu alinipiga chenga. Mara nyingi nilimwona kwa mbali. Mara chache nilikaribiana naye. Daima alirudi kinyume nyume, nami niliendelea kumfuata nikiongozwa na nguvu fulani* (uk .44).

Maelezo haya yanakaribiana sana na masaibu ya msimulizi katika safari yake ya kumsaka paa. Paa kama ***Nagona***, alionekana kwa mbali (kwa dalili za nyayo tu). Babu anapoendelea kusimulia msimulizi anasema kuwa nagona ni mwanga na kuwa:

> *Penye mwanga hukosi kupaona. Alipo, uwongo hujitenga, ni yeye peke yake aliyepo pale. Lakini hatakuruhusu umshike awe wako peke yako, maana ni wa kila mtu* (uk. 45).

Sitiari hii ya mwanga ambayo imemithilishwa na ***Nagona*** vilevile inasimamia ukweli. Kezilahabi analosema ni kuwa hakuna yule anayeweza kudai kuwa na ukiritimba wa maarifa na ukweli.

Msimulizi katika ***Nagona*** alipopigwa mieleka na mwanamke anaachiwa kitambaa alipokikunjua, katikati ya kitambaa hicho palikuwa pamenakishiwa kwa maandishi ya uzi wa dhahabu neno "nagona". Msimulizi anasema kuwa alilisoma neno hilo kwa shida.

Pana uhusiano mkubwa hapa baina ya maneno ya babu wa msimulizi kuhusu ugumu wa kumpata nagona na mwanamke ambaye msimulizi alimfuata akivuka milima, mabonde na misitu na hatimaye msimulizi hakumweka awe wake. Hivyo msimulizi ambaye kwa hali hii anasimamia binadamu, anashindwa kuudhibiti ukweli na kubaki katika giza lake la kutojua baada ya mshumaa wake kuzimwa na bundi, kukawa na giza. Huyu nagona amesukwa kutoka kwa lugha ya mwandishi (Kikerewe) ambalo (nagona) hutumiwa kwa mwanamke. Hili pia ni dhihirisho kuwa maana husukwa katika lugha kama nadharia ya Umuundoleo inavyosisitiza.

Sitiari nyingine inayowakilisha ukweli ni mwanga kwenye kitovu cha duara. Katika safari ya kumsaka paa (ukweli) mfalme ambaye ndiye angeridhisha kupatikana kwa paa alikuwa ameketi kwenye duara. Mfalme aliwaeleza kuwa:

> *Paa mnayemtafuta, anajua sana kucheza bao. Nataka acheze na mmoja wenu. Mkimshinda, basi mchukueni maana mtakuwa mmeshinda vikwazo vyote na mtakuwa mmeingia katika duara ya ukweli* (uk.33).

Kuingia katika duara hapa kunasawazishwa na kuupata ukweli. Babu wa msimulizi anampa mawaidha kuhusu siku ya ngoma kuu akisema:

> *Daima fuata duara na macho yako wakati wote yatazame katikati. Hicho kitovu kitakapopasuka, mengi yaliyofichama kwa karne nyingi yataonekana* (uk.46).

Siku ya ngoma kuu inapofika ambayo tayari nimeielezea kama jazanda, msimulizi anasukumwa kutoka katikati ya kitovu cha duara (ukweli ulipo) na watu wote waliogopa kukisogelea kitovu cha duara. Katikati ya duara ndiko kulikokuwa na mwanga uliowakilisha ukweli. Picha inayotokea ni ile ya ukweli kutofikika na binadamu hata anapotia juhudi za aina gani.

Huu ndio mwelekeo wa ki-Usasaleo unaosawiri ulimwengu kama pahali pabaya, ukweli kama kitu kisichoweza kufikika na sifa hizi zimeakisiwa kwa kiwango kikubwa na sitiari na taswira ambazo nimezielezea katika sehemu hii.

kiwango kikubwa na sitiari na taswira ambazo nimezielezea katika sehemu hii.

Kazi hizi mbili zimedengua mandhari (kutumia mandhari kwa namna ambayo haifungamani na hali halisi). Huu ni mseto wa fantasia na hali halisi ilivyo.

### 3:4 HITIMISHO

Katika sura hii tumezishughulikia sitiari na taswira alizozitumia Kezilahabi katika ***Nagona*** na ***Mzingile***. Tumeelezea kuwa mtindo wa kitaashira na kiistiari aliotumia mwandishi umesaidia kwa kiwango kikubwa kuyafafanua masuala ya kifalsafa muhimu anayoyashughulikia mwandishi katika kazi hizi mbili kama vile maisha na maana yake, msako wa mwanadamu wa kuutafuta ukweli na kule unakomwelekeza.

Aidha sitiari na taswira alizotumia pia zimetujengea picha ya ulimwengu kwa jinsi ambavyo Kezilahabi anavyouona na kuwa mtazamo huu umejikita katika nadharia ya Umuundoleo.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

# SURA YA NNE

# MWINGILIANOMATINI KATIKA *NAGONA* NA *MZINGILE*

## 4:1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulikia suala la mwingilianomatini kwa kuangalia jinsi ambavyo riwaya hizi mbili za Kezilahabi yaani ***Nagona*** na ***Mzingile*** zinavyoingiliana kimatini na matini nyinginezo za kifasihi. Mwingilianomatini ni dhana inayohusishwa na Julia Kristeva ambaye ni mnadharia wa fasihi. Mhakiki huyu anaamini kuwa matini yoyote ile ya kifasihi haiwezi kuangaliwa kivyake au kwa kujitegemea.

Aidha anasisitiza kuwa lazima kuwe na matini inayohusiana na nyingine kimtindo, kidhamira, muundo wa msuko au usawiri wa wahusika. Mwingilianomatini unasisitiza kuwa matini za kifasihi huingiliana na kuchangizana hivyo kuamini kuwa matini ya fasihi inajitegemea ni kupotoka.

Hata hivyo, maoni haya huwa hayamaanishi kuwa waandishi wa fasihi 'wanaiba' mawazo na mitindo kutoka kwa waandishi wenzao ila inamaanisha, kuwa mjadala ulio na maana, lazima uwe umehusiana na kitengo fulani ambacho tayari kipo na hata mawazo ambayo tayari yapo huwa yanaangaza au kukana mengine ambayo yameandikwa tayari.

Kwa msingi wa maelezo haya, tunaona kuwa riwaya hizi mbili za Kezilahabi zina elementi za kimwingilianomatini na kazi nyinginezo za fasihi. Baadhi ya elementi hizi zinahusiana na fasihi simulizi na hata fasihi

andishi hasa upande wa uhusika na sifa za wahusika wa kishujaa katika fasihi simulizi.

Aidha tutaangalia baadhi ya maudhui ya kazi hizi ambayo yanaingiliana na kazi nyinginezo za fasihi kama dini, kifo, ajali na athari za mifumo ya kiuchumi kwa ulimwengu wa tatu kwa jumla.

## 4:2 KUINGILIANA KWA *NAGONA* NA *MZINGILE* NA FASIHI SIMULIZI.

Katika riwaya ya ***Mzingile***, Kezilahabi ametumia kisa cha Kakulu (ambacho ni kisasili) kinachoonyesha msimamo wake kuhusu dini. Kisa hiki kina sifa kadhaa ambazo tunaweza kufananisha na zile za visa vya mashujaa katika fasihi simulizi hasa tendi. Kisa cha Kakulu kina maelezo yafuatayo: Kakulu alipozaliwa, kichwa chake kilitokeza kikiwa na ndevu nyingi zenye kuchanganyika na mvi, alipozaliwa tu, alikata kitovu chake kwa meno yake, akajipangusa maji na kuwakaripia wanaume waliokuwa hapo karibu. Baadaye katika kukua kwake, Kakulu aliweza kuzungumza lugha kadhaa bila kufunzwa kama vile Kiswahili, Kirusi, Kiarabu, Kiingereza na lugha nyingine nyingi.

Kisa hiki cha Kakulu kina sifa ambazo zinashabihi za visa vya mashujaa wengine katika tendi za fasihi simulizi ambapo shujaa azaliwapo huwa na ishara kwamba yeye ni shujaa. Vitendo vyake huwafanya walioko kumtambua kama shujaa kwa mfano Kakulu alipozaliwa aliwafokea wale waliokuwa karibu na alizaliwa akiwa tayari na meno. Mtume muhammadi alipozaliwa, tunaambiwa kuwa aliweka mikono yake juu ya ardhi na kuinua

kichwa chake akikielekeza juu ya mbingu kuashiria msingi wa utume na utukufu wake.

Shujaa Gautama naye alipozaliwa mito yote duniani ilikoma kutiririka ili maji yaweze kutafakari juu ya mtoto huyo.

Shujaa Mwindo alikataa kupitia kwenye uke kwa maana alidai kuwa huku kulikuwa mahali pachafu hivyo basi alipitia kwenye mbavu za mamake na alipozaliwa sawa na Kakulu, alitembea na kusema mara moja.

Tunapochunguza kisa cha Fumo Liongo tunaona kuwa, aliweza kusafiri umbali wa masafa ya siku nne kwa siku mbili peke yake, aidha aliweza kung'amua njama za maadui wake waliokuwa wamepanga kumwua hata bila ya kuambiwa na labda muhimu zaidi asingeweza kuuliwa ila kwa njia moja tu ambayo ni kudungwa kitovu kwa sindano ya shaba. Hivi ni vitendo vinavyomfanya shujaa kutambuliwa kama shujaa kama vile tumejadili kumhusu Kakulu hapo juu.

Kisa cha Kakulu kinazo sifa nyinginazo za kishujaa kama vile kutolelewa na wazazi wake kwa kuwa tunaambiwa kuwa mamake Kakulu alipoona kuwa meno yamemjaa Kakulu mdomoni mara tu baada ya kuzaliwa, alifunga virago vyake na kumtoroka. Shujaa Muhamadi naye alinyonyeshwa na kulelewa na mtu mwingine kabla ya kurudishwa kwa mamake.

Mashujaa pia huenda kwenye pori au milima kuishi kwa upweke kwa mfano Kakulu alienda kuishi maisha ya upweke mlimani baada ya kuwafunza wazee watano kuhusu historia, mila, desturi na dawa. Hizi zote ni sifa za

kishujaa kama vile zinavyosimuliwa katika fasihi simulizi. Isa Masihi aliwaacha wafuasi wake na kwenda jangwani kwa muda wa siku arobaini ili kufunga na kuomba.

Mutiso (1985) anaelezea baadhi ya sifa za Majagina kuwa wanafanya mambo yasiyokuwa ya kawaida kwa mfano, Kakulu kuweza kuongea hata akiwa bado tumboni mwa mamake na mara tu baada ya kuzaliwa. Tunaona kuwa maisha yake ni ya upweke. Kakulu hakuoa na watu wa kijiji chake hawakumwelewa. Aidha mashujaa wengine kama vile Isa Masihi na Fumo Liyongo hawakuoa. Hivyo mashujaa hupenda maisha ya utawa na usufii.

Mashujaa hukuza utamaduni wa watu wao kwa kuwafunza historia, mila, desturi na dawa. Prometheusi ambaye ni shujaa wa Kiyunani aliiba moto na kuwapelekea Wayunani. Kunguru ambaye ni shujaa wa Kihindi naye aliiba moto na kupelekea makabila ya Kihindi ya Kaskazini Magharibi. Liongo naye aliwaachia watu wake (Waswahili) gungu. Naye Kakulu aliwafunza wazee watano kuhusu historia yao, mila,desturi na dawa.

Tunaona kuwa mpaka kati ya Mungu na shujaa ni mwembamba sana kwa mfano; Kakulu kuwateua wazee watano na kuenda nao msituni kuwafunza ni mshabaha mkubwa na Yesu Masihi kuteua wafuasi wake kumi na wawili- ambao pia aliwafunza na hatimaye Kakulu aliwaamrisha hao wazee baada ya kuwafunza akisema:

> *Sasa nendeni; waongozeni na wafundisheni watu*
> *Niliyowafundisha* (uk. 3).

Haya maagizo ni sawa na yale ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake katika kitabu cha Matendo ya Watumwa katika Biblia. Aliwaambia:

> *"Roho Mtakatifu akija mtapata uwezo na mtawafundisha watu Yerusalemu Samaria na ulimwenguni kote."(*Matendo ya mitume 1:8)

Katika *Mzingile* kuna mfano wa kisa anachotolewa msimulizi na mzee kuelezea kwa nini mzee hakuwa anataka tena kuhusishwa na muundo uliokuwapo ambacho pia mfano wa mughani katika fasihi simulizi mzee anamsema:

> *Nilipokuwa kijana nilikuwa mpiga mieleka hodari. Hapakuwa na yeyote alieweza kunitupa nje ya duara.*
> *Nilishikilia kitovu hiki karne hadi karne hadi siku moja kichaa mmoja katika ndoto zake aliwaambia washindani wangu siri ya kivuli changu. Hiyo ndoto ya kichaa ilifichua siri ya nguvu zangu. Walipopiga kivuli changu kwa fimbo, nguvu ziliniishia nikaanza kuwa mzee kadiri wakati ulivyopita* (uk. 13).

Kisa hiki cha mzee aliyekuwa shujaa na kupoteza nguvu zake baada ya kusalitiwa na 'kichaa' kinashabihiana na kisakale au Mughani wa Lwanda Magere ambaye ni shujaa wa jamii ya wajaluo. Lwanda Magere anasimuliwa kuwa alikuwa shujaa ambaye aliweza kupigana vitani na kuwashinda maadui wa Wajaluo peke yake. Inasemekana kuwa kila alipoenda vitani hakuna mshale wala mkuki uliowaza kupenya ngozi yake. Maadui wa Wajaluo wa Sidho ambao walikuwa Walang'o walipanga njama ya kumwoza msichana wao mrembo kwa Magere ili aitafute siri ya nguvu zake za ajabu.

Ingawa mke wa kwanza wa Lwanda Magere alimshauri asimwoe binti huyu, alimpuuza na kumwoa. Hatimaye, binti huyu alipoifahamu siri ya nguvu za

Lwanda Magere aliendа kwao na kuwafichulia wazee wake siri na Lwanda Magere akaangamizwa kwa kivuli chake kupigwa kwa mkuki.

Visa hivi viwili ni mfano mwingine mwa mwingiliano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Hapa tunaona kuwa shujaa anasalitiwa na zile nguvu zake za kiajabu kujulikana kupitia kwa usaliti huo na kusababisha kuanguka kwake.

Aidha Kineene anavyosema kuwa mashujaa huweza kudhuriwa mahali hii pamoja kwa hali kivuli cha mzee kilipopigwa fimbo nguvu zilianza kumwishia, Lwanda Magere naye aliangamizwa kwa kivuli chake kuchomwa kwa mkuki. Fumo Liongo vile vile kwa kudungwa kwa sindano ya shaba kwa kitovu chake. Aidha Kakulu alipobaki mlimani baada ya kuwafunza wazee aliowafunza kuenda kuongoza na kufunza watu aliyowafunza, alibaki na hakuonekana tena.

Mshabaha mwingine uliopo katika visa hivi ni kwamba kuna mtu mwingine ambaye huweza kupata habari kuhusu asili ya nguvu za shujaa na huzielezea ndipo anapohasiriwa. Katika ***Mzingile*** pia kuna mfano wa kisa kinachoingiliana na fasihi simulizi. Akimwelekeza njia kipofu aliyekuwa msimulizi alimsimulia kuhusu asili ya upofu wake. Anapoanza kusimulia jinsi alivyokuwa hadi hatimaye akawa kipofu, anasema:

> *Hadithi yenyewe ilianza hivi.*
>
> *Nilizaliwa nusu kipofu kutokana na magonjwa ya zinaa aliyokuwa nayo mama yangu.*

Mwanzo wa masimulizi haya unashabihi mianzo ya hadithi. Mwanzo kama huu unahusisha hadithi hii na hadithi nyingine na unatuweka katika hali ya matarajio ambayo huwa kawaida katika hadithi hata karibu kutuhakikishia kupata funzo kutokana na hadithi yenyewe. Funzo la hadithi hii hata analitoa mzee huyu kipofu kabla ya kuanza kuitamba hadithi yenyewe. Anasema:

*Ni kwa kuwa palipozibwa ndipo penye njia kweli.*

Mhusika huyu vile vile ana sifa za kishujaa ambapo yeye pia hata kama ni kipofu ndiye anayemwongoza msimulizi njia. Huyu mzee ana maarifa mengi.

Anapoendelea kusimulia kuhusu maisha yake anafikia sehemu ambapo anaimba wimbo ambao kama anavyoelezea babake mlezi alimhimiza aimbe kama njia ya kujitafutia riziki. Nyimbo hutumiwa katika simulizi au hadithi katika fasihi simulizi ili kusisitiza au kuonyesha kiini au wazo kuu katika hadithi inayohusika.

Wimbo huu ambao ulikuwa unaelezea tanzia ya binadamu ulielezea baadhi ya matatizo ambayo kwamo binadamu amejitumbukiza kama vile vita, hatari ya mabomu ya kinyuklia na utupu wa maisha kwa ujumla.
Ni muhimu hapa kuona kuwa katika wimbo huu, ule mtazamo wa ki-Usasa ambao kazi hii inaoinishiwa umejitokeza hasa kukata tamaa.
Ulimwengu hapa umedhihirika kama mahali pabaya na binadamu kama kiumbe anayejikuta katika hali ya kukata tamaa kutokana na mvurugiko wa maisha yake. Mzee kipofu anasema katika wimbo wake:

*Wanaojidai kuona wametufikisha Ukingoni mwa bahari yenye papa na nyangumi,*
*Na wanatushauri tuogelee katika mihadhara.*
*Ambayo vichukua sauti vyake ni mitutu ya bunduki*
*Na viti vyake ni vichwa vya nyuklia* (uk. 28).

## 4:3 *NAGONA* NA *MZINGILE*, *PEDRO PARAMO* NA *BABU ALIPOFUFUKA*

Kazi za Kezilahabi yaani ***Nagona*** na ***Mzingile*** zinashabihiana kwa kiasi kikubwa na riwaya iliyoandikwa na mwandishi wa Mexico anayejulikana kama Juan iitwayo ***Pedro Paramo***. Waandishi wote wawili wametumia sitiari ya safari kuonyesha juhudi za binadamu katika kujitafuta na kuitafuta maana ya maisha yake.

Katika kazi hizi zote tatu kuna matumizi ya taswira ya msafiri kupotea njia. Katika ***Nagona*** msimulizi anasema:

*Kama huo ndio ulikuwa mwanzo wa safari yangu, sina hakika (*uk.1).

Katika ***Mzingile***, msimulizi ambaye ametumwa na walimwengu kwenda kumwambia Mungu kuwa wamemuua mwanawe, mkombozi wa pili anapoanza safari hii hajui aelekea wapi: Taswira hii ya msafiri kutojua anakoelekea akiwa safarini kutafuta ukweli aidha inajitokeza katika ***Pedro Paramo***. Juan Preciado ambaye ndiye mhusika mkuu wa kazi hii pia yu safarini kumtafuta babake kulingana na maagizo aliyopewa na mamake kabla ya kifo chake. Anapofika mji wa Comala, Mexico hana hakika na

hajui afuate njia gani. Inambidi kuuliza kijana mmoja ambaye inasadifu kuwa ni mwanaye Pedro Paramo pia.

Katika mifano hii yote tunakabiliwa na wazo kuwa maisha ya binadamu ni batili. Ukweli nao unaonekana kuwa mgumu kufikika ingawa binadamu yu katika harakati za kuutafuta. Katika ***Nagona*** jitihada za msimulizi kumtafuta 'paa' akisaidiwa na wasaidizi wake hazifui dafu. Hata anapompata huyu 'paa' hatimaye, hawezi kumweka awe wake. Anampiga myeleka na kumtoroka.Katika ***Mzingile*** msimulizi anaikwea milima yenye majabali, miteremko mikali mikondo ya maji mikali na hata misitu yenye miba.

Katika ***Pedro Paramo***, Juan anaelekezwa kwenye nyumba ya mwanamke anayeitwa Dona Eduviges ambaye angempa mahala pa kulala. Akiwa katika nyumba hii anaota mambo ya ajabu kuwa alikuwa akiona mizuka na kusikia sauti za wafu. Maajabu haya yanapoendelea, Juan hatimaye anagundua kuwa hata Eduviges pia ni mfu. Kama alivyo Juan Preciado mwenyewe.

Taswira hii maajabu safarini na mizuka inashabihi maajabu anayokumbana nayo msimulizi katika ***Nagona*** mwanzoni mwa safari yake.

Msimulizi huyu anapoanza safari yake anasikia mtu akitembea lakini hawezi kumwona. Anastukia akipigwa viboko matakoni na mgongoni lakini haoni anayempiga.

Waandishi hawa wawili wametumia safari kuonyesha vile maisha yamekosa maana na kuwa ni ya mzunguko. Jitihada za Juan kumtafuta babake zinamfafanulia kuwa Pedro Paramo (babake) alikuwa amewakandamiza

watu wa Comala. Ardhi karibu yote Comala ilikuwa mali yake na kuwa aliwanyanyasa watu wa Comala sana.

Haya ni masuala yanayoonyesha hali za kiuchumi za nchi za ulimwengu wa tatu. Tofauti iliyopo baina ya Rulfo na Kezilahabi ni kuwa, Kezilahabi anaangalia chumi za ulimwengu wa tatu kwa jumla na vile zimeporomoshwa na ubepari na ukoloni lakini Rulfo anazingatia nchi mahsusi yaani Comala, Mexico ambayo ni nchi ya ulimwengu wa tatu.

Katika ***Nagona,*** safari ya kufanyia viwanda utafiti ili kujua kiini cha kuporomoka kwao inafichulia msimulizi ukweli kuwa maji yanayotoka kwenye viwanda yenye sumu kali yalikuwa yameharibu maji ya kunywa, viwanda vingi vilikuwa magofu sasa, majengo yaliyokuwa mazuri yalikuwa yamezungukwa na madimbwi ya maji machafu. Baiskeli zilizokuwa zikitengenezwa zilikuwa hazina breki. Taswira hizi zote zinaonyesha hali ambapo binadamu ni kama anajitayarishia majanga. Hali inayozuka dhamira ya kukata tamaa. Hapa tunaona kuwa juhudi anazofanya mwanadamu ili kujiendeleza apate furaha ndizo zinazomtumbukiza katika maangamizo. Mathalani anajenga viwanda kufuatia uvumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia lakini hivi vyote vinautilia ulimwengu sumu inayosababisha maafa.

Hii ndiyo taswira inayomshughulisha Rulfo pia. Hata ingawa Pedro Paramo alijitahidi kutafuta mali kwa kunyanyasa watu Comala, mwenyewe hakupata furaha yoyote. Tunaelezwa kuwa hangemkubalia yeyote kumwekea kikwazo katika jitihada zake za kutafuta mali. Hata angeleta mashtaka kwa yeyote ambaye hakukubaliana na jinsi alivyofanya biashara yake (uk. 35-39). Hata

Padri Renteria anaidhihirisha matendo yote maovu kama unyakuzi wa ardhi ambazo hazikuwa zake.

Hali hii ya asasi za utawala za nchi hasa mahakama kutumiwa vibaya na viongozi kwa maslahi yao ni taaswira ya mataifa ya ulimwengu wa tatu kunyonywa kiuchumi na mataifa yaliyoendelea.

Katika ***Nagona*** Kizee kilichokuwa kinaelekeza msimulizi na wenzake kiliwafikisha sehemu ambako vinyesi vilikuwa vimepangwa kandokando ya njia na kiliwaeleza hivi:

> *Humu mwote ni mahali walipozikwa wafalme wa Uingereza, Ureno, Watawala wa Ufaranza na maraisi wa Marikani. Palikuwa mahali panapoheshimika sana. Lakini vichaa fulani waishio katika bonde lile huja hapa kujisaidia.*
>
> *Wanasema wanaondoa hasira yao iliyokuwa imegandamizwa makooni mwao kwa miaka mingi na nguvu za kiuchumi.*

Taswira nyingine ni ya viongozi kukosa kuelekeza mataifa yao vizuri pia inajitokeza katika ***Mzingile***.

Kijana aliyekuwa anaishi bondeni anamwelezea msimulizi jinsi ambavyo viongozi wa kisiasa walivyoshindwa kuendeleza uchumi wa nchi yao kwa kuwa na tamaa kupita kiasi. Anasema:

Ni viongozi wa chama ndio waliokuwa wa kwanza kulewa heshima. Hawa wakataka watu wote nchini wawe vikaragosi vyao.

Hii ni picha sawa na alivyofanya Pedro Paramo Comala ambapo kila fujo, uovu na ufisadi unahusishwa na Paramo kwa mfano Dorotea ambaye mwanaye alifariki dunia anakula njama na Paramo wamtafutie mwanaye

Miguel wanawake. Paramo pia anang'ang'ania mapenzi ya Susana ambayo hapati kwa kiwango kile alichotaka na hatimaye kifo cha Susana kinamfanya Paramo aufunge mji wote na hata kilimo kuharamishwa. Haya yote Paramo anayafanya kwa usaidizi wa wa Padri Renteria. Iwapo kanisa inaruhusu ufisadi kutekelezwa bila ya kutoa pingamizi yoyote basi hali ilikuwa imeoza kweli.

Haya ndiyo Euphrase Kezilahabi anasema kuwa hatimaye yaliwafanya wengi wa watu kufyata mkia na wataalamu wakaacha jahazi liendeshwe na upepo na katika kuyumbayumba watu wakagonga mwamba.

Hali hizi zinaonyesha uduni wa maisha ya mwanadamu na vile anakabiliwa na ugumu wa kung'ammua anakoelekea. Katika ***Nagona, Mzingile*** na hata ***Pedro Paramo***, tunaona binadamu amejitokeza kama kiumbe dhaifu kisichoweza kuudhibiti ulimwengu; hawezi kuufanya umtumikie ili kumletea furaha.
Msimulizi katika ***Nagona*** anafanya bidii kumtafuta 'paa' (ishara ya ukweli). Anamsaka hadi anampata na anapompata, paa anampiga myeleka na kumwacha akitapatapa.

Katika ***Mzingile***, msimulizi ambaye yu safarini kumtafuta 'mzee' ili aende kumzika mwanawe; anakumbwa na matatizo chungu nzima na hata anaporudi hajafaulu kumpata mzee amzike mwanaye.

Katika ***Pedro Paramo***, juhudi za Paramo kujilimbikizia mali hazimpi raha yoyote. Hata kama ana ardhi nyingi na mali, hana raha maana yule anayempenda (Susana) hawezi kurudisha penzi lake. Maisha kwake yamejaa

upweke na kukata tamaa.Kwa hali hii, kazi hizi zinaingiliana kimaudhui hasa upande wa maana ya maisha.

Uduni wa maisha katika kazi hizi tatu unatiliwa mkazo na kuwepo kwa zogo. Katika maisha ya wahusika katika ***Mzingile,*** kuna mitambo hatari ambayo imebuniwa na binadamu mwenyewe na sasa inatishia maisha yake. Katika ***Nagona*** ajali ya mitambo ya kinyuklia inatokea na kusababisha maafa makubwa. Taswira hii ya vurumai inafikia kilele chake katika ***Nagona*** wakati wa Ngoma kuu. Watu wote (wanafalsafa, wanasaikologia na wanamapinduzi) wanashiriki katika vurumai.

Katika ***Pedro Paramo***, Fulgor Sedano ambaye ni msimamizi wa Media Luna na ambaye pia alimsaidia Pedro Paramo kuipata ardhi yake kwa njia ya ufisadi anauawa katika vita vya mapinduzi. Hali hii ya kukatisha tamaa pia inajitokeza katika ***One Hundred Years of Solitude***.Katika riwaya hii, mhusika kaneli Aureliano Buendia anajaribu kubadili hali ya kisiasa ya Macondo. Anapanga na kusimamia vita thelathini na viwili.ambapo wanawe wa kiume wote kumi na saba wanaangamia. Hali kadhalika majaribio ya kisayansi ya Jose Arcadio Buendia yanapokosa kufua dafu, Jose Arcadio anakuwa mwendawazimu na anaishi akiwa amefungiwa chini ya mti.

Maoni haya yote yanadhihirika kuwa mwandishi haandiki kwa ombwe tupu bali matini za kifasihi huingiliana kwa kiwango kikubwa kama nadharia ya mwingiliano inavyosisitiza

## 4:4 DINI

Katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** Kezilahabi anakuza wazo kuwa dini haitoi suluhisho kwa matatizo yanayomkabili binadamu maishani. Mtazamo huu ni motifu ya kidhamira inayojitokeza katika maandishi ya Kezilahabi kwanzia riwaya ya ***Rosa Mistika***. Dini inasawiriwa kama inampa binadamu suluhu ya muda tu kwa matatizo yake. Licha ya haya, dini inaelekea kuwa kikwazo kwa binadamu na jitihada zake za kuutafuta ukweli. Hata katika ***Gamba La Nyoka*** Kezilahabi anaona imani ya dini kama kizuizi cha binadamu kutafuta suluhhisho katika fikra. Mwenyekiti wa kijiji cha Kisole anasema:

> *Ndugu wanakijiji wazee walisema 'Mungu' anakulinda na wewe unajilinda. Kitendo ambacho tumekata shauri kukitenda ni cha kishujaa. Tusitegemea tu kuwa Mungu yupo. Tujiandae* (uk.19).

Ni kama Mungu ni kizuizi kwa ushujaa wao. Katika ***Nagona***, Babu anasema hivi kuhusu "mwana wa Mungu- Mkombozi",

> *Alipotea njia karne nyingi zilizopita.*

Msimulizi anapoendelea na safari yake anaingia kwa nyumba ya Padri ambaye ni mlevi ajabu. Hana kinywaji kingine kwake isipokuwa mvinyo. Hata siku ya Ngoma kuu hakuudhuria maana alikuwa amelewa chakari. Hata tunaarifiwa kuwa alikunywa mvinyo hadi akafa. Hii ni kejeli kubwa kwa dini ambayo inapaswa kuwa mwelekeo kwa watu na viongozi wa kidini wanapaswa kuwa mfano mwema kwa wafuasi wao na watu kwa jumla.

Aidha katika ***Mzingile***, Padri amesawiriwa kukosa kutoa mwongozo kwa watu. Ukame ulipoingia nchini alianza kusali lakini haukuisha. Na alipokata tamaa alianza kumtukana Mungu huku akivunjavunja masanamu kanisani.

Si dini ya ukristo tu ambayo haitoi suluhu za matatizo hata uislamu pia. Sheikh naye anaingilia anasa za kujiolea visichana vidogo vidogo baada ya kushindwa kushugulikia matatizo.
Msimulizi katika ***Mzingile*** anasema;

> *Binadamu walipoanza kulana wenyewe kwa wenyewe, msikiti uliota nyasi hata paani. Nguvu za kujitafutia chakula zilipomwishia mahurulaini walimkimbia Sheikh.*
> ( uk. 20)

Katika kisa cha Kakulu hasa sifa zake za kishujaa zinaelekea kutilia shaka wazo la Mungu na nafasi ya dini kwa kuwa msimulizi katika ***Mzingile*** anapomaliza kusimulia kisa hiki anasema:

> *Je inawezekana kuwa ndoto za karne ishiruini zilizoongozwa na kisasili zimefika ukingoni? Na kelele za kichaa aliyetaka kujenga historia mpya zimekwama? Yaelekea inabidii kisasili kingine kianze na ndoto mpya!*

Msimulizi anayasema haya baada ya kuhitimisha kisa cha Kakulu kwa kusema kuwa hatimaye Kakulu alikuwa Kisasili, akawa mwanzilishi wa taifa, akawako daima. Akawa kweli. Ikaenezwa ulimwengu mzima. Upo uwezekano mkubwa kuwa Kezilahabi anatilia dini na nafasi yake katika jamii shaka. Hata baadaye katika ***Mzingile***, msimulizi anaendeleza wazo hili la kutilia dini shaka kama njia ya kuleta suluhu kwa matatizo ya kinadamu.

Msimulizi pia anasema kuwa walipotembelea gofu alimoishi Padri walipata Biblia, Kurani na Kamusi na baada ya kuvipitia waliona kuwa vitabu hivyo havikuwa na maana tena. Dini inatiliwa shaka na Kezilahabi.

Mtazamo huu wa dini kukosa kutoa mwelekeo kwa masuala yamhusuyo binadamu unatiliwa mkazo na Rulfo katika ***Pedro Paramo***. Renteria ambaye ndiye Padri wa mji wa Comala hawezi kuwafanya waliokufa wakatulia katika ufu wao.Tunaona kwamba wale waliokufa bila imani wanauzunguka mji huu kama mizuka wakitafuta wokovu. Hivi kazi ya kuwaomba msamaha wa dhambi dakika ile wanapokaribia kifo, Padiri haitekelezi.

Si jukumu hili tu ambalo Padiri huyu Pedro Paramo hatekelezi bali hatumwoni akishutumu maovu anayoendeleza Paramo ama akipigania haki za wale wanaonyanyaswa na Paramo kama inavyostahili kuwa. Kwa kweli anachokifanya ni matendo mabaya ya Pedro Paramo.

Katika kazi hizi zote tatu, dini imeonekana kama asasi mojawapo ya binadamu ambayo imeshindwa kutoa jawabu toshelevu kwa matatizo ainati yanayomkumba mwanadamu. Picha hii tunaweza kusema kuwa mbali na kudhihirisha mkondo wa kimaandishi wa Usasa na Usasaleo, inaweza kuafiki uhalisi wa maisha wa karne mbili zilizopita za ulimwengu wa tatu kwa jumla.

Katika kipindi hiki, uozo wa dunia umefikia kilele chake kwa kuvishwa vazi jipya la utandawazi; na matokeo yake yamekuwa mauaji, ubaguzi wa rangi, ufilisi wa uchumi wa nchi za ulimwengu wa tatu na uangamizaji wa imani za

kidini kwa jumla. Hii ndiyo taswira ambayo imeingilia masuala ya kidini vilevile. Kama vile tumeelezea hapo juu, dini imeshindwa kutekeleza jukumu la kuleta amani na upendo ulimwenguni kote.

## 4:5 USAWIRI WA WAHUSIKA NA MAZINGIRA

Mwingilianomatini mbali na kudhihirika upande wa maudhui umetokea pia upande wa usawiri wa wahusika na usawiri wa mandhari Katika sehemu iliyotangulia ambayo tumeelezea kuhusu baadhi ya elementi za fasihi simulizi ambazo zimejitokeza katika kazi hizi mbili za Kezilahabi tumeweza kuelezea namna ambavyo mhusika Kakulu alivyo na sifa za kishujaa za mashujaa wa fasihi simulizi.

Katika sehemu hii tutaangaza kwa undani zaidi uhusika katika kazi hizi kwa kuzingatia dhana ya umwingilianomatini. Wamitila anasema:

> *Wahusika katika hadithi hufanana na binadamu lakini si binadamu.Kazi ambazo zimeandikwa katika misingi ya "uhalisia wa kirasimi" huwa na sifa ya mfanano mkubwa kati ya wahusika na binadamu kuliko kazi zilizoandikiwa mitindo ya kimajaribio au ki-Usasa kama* ***Nagona*** *na* ***Mzingile*** *(*uk.18).

Kwa kuwa ***Nagona*** na ***Mzingile*** ni kazi ambazo zimeandikwa katika msingi wa ki-Usasa na Usasaleo, tunaona kuwa hii kanuni ya kiuhalisia ya wahusika kusawiri binadamu imepuuzwa. Hivyo tunachokiona ni kuwa wahusika katika kazi hizi mbili hawaishi katika ulimwengu unaolingana moja kwa moja na ulimwengu halisi. Wakati mmoja msimulizi yu hai lakini wakati mwingine ni mfu.

Katika ***Nagona***, msimulizi akiwa katika safari ya kutembelea viwanda anaambiwa na kizee kuwa walitumia miaka kumi kufika pale walipokuwa. Kizee kinamwambia:

> *Miaka kumi. Miaka kumi kufika hapa! Na ingechukua muda mrefu zaidi kama ndege yenu isingeanguka na kuteketea. Ajali hufanya mambo yawe.*

Ingawa kifo cha msimulizi hakielezwi wazi hali yake inaelekea kuwa imebadilika. Ni vigumu kupambanua baina ya mazingira ya ufu na uhai ndiposa katika sehemu ya mwanzo ya kazi hii msimulizi anasikia sauti za vicheko lakini haoni watu.

Katika ***Mzingile*** kipofu anayemwongoza msimulizi njia anamwelezea kuwa hali yake ilivyokuwa wakati huo ilikuwa tokeo la ajali. Anamwelezea msimulizi akisema:

> *Dreva mlevi ndiye aliyenihamisha sehemu hizi. Ndiye aliyeniwezesha kuvuka ule mstari unaoogopwa na wengi* (uk.29).

Msimulizi anashangazwa na maneno haya na anamwuliza kipofu:

> *Unataka kuniambia kuwa ninazungumza na mtu Aliyekufa* (uk. 29).

Picha hii ya wahusika walio hai kuweza kuongea na kuwasiliana na wahusika waliokufa tayari pia inajitokeza katika ***Pedro Paramo.***

Juan Preciado anapoelekezwa kwa nyumba ya Dona Eduviges ambako anatarajia kupata mahali pa kulala, usiku mzima anavamiwa na sauti za kutisha zisizo za kawaida hata katika ndoto zake. Anapogutuka kutoka usingizini, Juan anaenda kumtafuta Eduviges ambaye anaanza kumwelezea kuhusu mamake. Polepole Juan anaanza kugundua kwa mshangao mkubwa kuwa Eduviges hayuko hai, ni mzuka. Ukweli ni kuwa Juan alikuwa akiishi na kuzungumza na mzuka. Anapogundua hivi anaamua kutoka kwa Eduviges lakini anagundua mwishowe kuwa 'watu' wote wa mji wa Comala ni mizuka.

Juan mwenyewe hatimaye anajifunza mambo mengi lakini anayaelewa zaidi akiwa mfu (baada ya kujiua). Hata anaendelea kusimulia hadithi baada ya kufariki. Huu ni mshabaha mkubwa na vile msimulizi katika ***Mzingile*** anavyogundua mengi katika safari ya kifikra akiwa mfu kwa mfano kuhusu matatizo ya nchi ya kiuchumi. Sifa hii pia inajitokeza katika riwaya ya ***Bina -Adamu*** ya Wamitila.

Siyo kazi hizi tatu zilizo na wahusika zilizo na wahusika waliosawiriwa kwa njia isiyo ya kawaida bali hata ***One Hundred Years of Solitude*** pia ina mtindo huu. Mhusika Melqueiades anarudi kuishi kwa Buendia na kushiriki katika maisha ya kawaida.
Katika ***Babu Alipokufa***, Babu ambaye alikuwa amefufuka anamjia mjukuu wake 'K' na kumpeleka kwenye dunia ya pili ambapo anamwonyesha jinsi alivyoshiriki kuharibu taifa yake. Mwishowe anaporegeshwa katika ulimwengu wake hakuweza kukabiliana na mabadiliko yaliyompata hivyo anajinyonga. Baadaye anajigeuza mzuka kama Babu na hata kuwajia waliohai kama vile watoto wake.

Tunaweza kusema kuwa kazi hizi katika kuvunja muundo wa kikawaida zinakuwa kama isitiara ya miundo ya mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya ulimwengu. Ni kama msomaji anaachwa baada ya kusoma kazi hizi akitafakari kama uhai unaomzingira kweli upo au ni kifo tu kilichopo. Aidha kazi hizi zinatuchochea kutafakari kuhusu ukweli na uhalisi tunaoujua.

Msimulizi katika ***Pedro Paramo*** anasema:

> *Hamna kumbukizi ambayo inaweza kudumu milele, kumbukizi zote daima hutowek* (uk. 93).

Wazo lingine linalohusu wahusika ambalo linatokea katika kazi hizi zote ni upweke wao wa maisha yao. Msimulisi katika ***Mzingile*** anasema:

> *Nilitembea harakaharaka kuelekea hapo nikimeza mate mara mbilimbili. Nilipomkaribia nilimrukia juu kumkumbatia na kumpapasa hali nikisena kwa sauti "Nakupenda" karne na karne nikikutafuta wewe!* (uk. 8).

Pia anaendelea kusema:

> *Pale nilipoangukia hapakuwa na mtu. Palikuwa na mchanga uliokuwa kama tuta. Hakuna nilichoshika, isipokuwa mchanga.*

Hata katika ***Nagona*** hali si tofauti na hii. Msimulizi baada ya kumpata 'paa' (ukweli), anampiga myeleka na kumwacha peke yake.

Katika ***Pedro Paramo***, Juan anagundua kuwa babake (Pedro Paramo) aliachwa kwa upweke mkubwa wakati mkewe (Susana) aliyekuwa ameishi naye kwa muda mfupi alishikwa na uwenda wazimu kisha akafa.

Upweke huu wa wahusika tunaweza kusema kuwa unasawiri kwanza kabisa kilele cha msako wa kifikra kama ilivyo katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** lakini pia ni hali ya kijumla inayosawiriwa ya upweke wa mataifa ya Amerika Kusini na Afrika kwa jumla; mataifa ambayo yametengwa kwa kunyonywa kiuchumi na mataifa mengine na pia yamejitenga kwa kukosa kutimiza majukumu yao ipasavyo hasa viongozi na asasi za utawala.

Wazo hili la upweke pia ni elementi ya ki-Usasa ambapo binadamu anasawiriwa kama kiumbe anayeishi katika ulimwengu usiomjali, amezungukwa na mateso na ubwege na anashindwa kukabiliana au kupatana vyema na uhalisi wa mambo.

Mandhari nayo yamesawiriwa kwa njia isiyo ya kawaida katika kazi hizi. Mandhari katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** si Mandhari ya kiulimwengu. Ni mazingira ya kindoto baina ya kifo na uhai.
Katika ***Nagona*** msimulizi mara nyingi anajipata katika mazingira ya bondeni, mahali ambapo pametawaliwa na ukungu na maluweluwe. Bonde na giza ni ishara ya matatizo katika kazi nyingi za kifasihi.

Katika ***Mzingile*** msimulizi anapitia msituni, majabalini na miteremko mikali. Mandhari kama haya katika fasihi ya ubwege huashiria maisha kama duni, ya kinasibu na ya kukatisha tamaa. Katika riwaya ya ***Pedro Paramo*** Mandhari ya bondeni pia yamo. Hata Susanita anasikika akiomboleza kutoka maziarani mahali ambapo pamejaa vumbi. Mandhari aidha ni ya gizagiza. Mandhari haya ya gizagiza pia yanatokea katika tamthilia ya Samuel Beckett ya ***Waiting for Godot***. Haya mazingira yanazua hisia za

huzuni na kukata tamaa. Katika kazi hizi zote dunia inaonyeshwa kama mahali pa mateso na maafa mengi.

## 4:6 MBINU NYINGINE ZA KI-USASALEO/UMUUNDOLEO

***Nagona*** na ***Mzingile*** ni hadithi ambazo zimesimuliwa katika nafsi ya kwanza. Matumizi ya viwakilishi 'mimi' na 'ni' yemetokea sana katika kazi hizi mbili na hivyo kuchangia kufupisha masafa yaliyopo kati ya mhusika na msomaji. Riwaya hizi zinatumia masimulizi ya kifantasia yanayokiuka uhalisi wa kawaida huwa na athari kubwa katika usimulizi wa nafsi ya kwanza. Msomaji anahisi kuwa karibu sana na msimulizi na anajitambulisha na matendo na hisia za msimulizi.

Msimulizi katika ***Nagona*** anapoanza safari anasema :

> *Kichomi kilianza kuniuma ubavuni.*
>
> *Nilipiga magoti chini kwa maumivu nilianza kutembelea magoti. Nilisikia vicheko vya watu (uk. 1).*

Huu ni mfano wa mbinu ya "Mkondo wa ung'amuzi" anavyoiita Wamitila ambapo maelezo yanayompitikia mhusika akilini. Mawazo ya ndani aliyonayo mhusika yanawakilishwa kwa mapana na marefu.

Katika ***Mzingile*** msimulizi anautumia mtindo huu pia anasema:

> *Jua lilipotua, nilikuwa nimeshuka chini bondeni. Kulikuwa na kiupepo kidogo lakini hapakuwa na dalili ya maji. Kwa kuogopa kupotea njia nilikata shauri kutafuta pahali pazuri pa kulala* (uk. 8).

Nyingi za sehemu za usimulizi wa riwaya ya ***Pedro Paramo*** zimefanywa katika nafsi ya kwanza na nyingine zimefanywa katika nafsi ya tatu.
Katika masimulizi anayotumia Juan Preciado, tunaweza kuona kupitia kwa jicho lake na hata kuzisikia sauti anazozisikia za wafu na hata tunaweza kuona picha ya maangamizi ya mji wa Comala yale ambayo Juan anaweza Kuyaona kupitia kwa jicho la wale. Waliokufa anapofika Comala ni jazanda ya mabadiliko yaliyokumba Amerika Kusini (Mexico).

## 4:7 HITIMISHO

Katika sehemu hii tumeshughulikia baadhi ya vipengee vya mwingilianomatini katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** na matini nyingine za fasihi.

Tumeona vile baadhi ya wahusika katika kazi hizi wanaweza kulinganishwa na wahusika katika fasihi simulizi hasa mfano wa Kakulu na sifa zake zinazokaribiana na zile za mashujaa wa hadithi kama ile ya Fumo Liongo.

Tumeshughulikia pia baadhi ya maudhui ambayo yanashabihiana katika riwaya za ***Nagona***, ***Mzingile, One Hundred Years of Solitude*** na hata ***Babu Alipofufuka***.

Kinachodhihirika wazi hapa ni kuwa fasihi ya Kiswahili imechukua mahali pake katika fasihi nyingine za ulimwengu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5:1 MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU

Katika tasnifu hii tumeshughulikia riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** za Euphrase Kezilahabi ambapo mbali na kuonyesha vile ambavyo zinavyoingiliana na kutofautiana na kazi zake za awali za kinathari, pia tumeshughulikia sitiari na jazanda zilizomo katika kazi hizi na vile zimefanikisha maudhui yake.

Katika sura ya pili tumehakiki kwa muhtasari kazi za Kezilahabi za kinathari kazi zilizotangulia ***Nagona*** na ***Mzingile*** kwa nia ya kuzilinganisha na kuzitofautisha. Katika riwaya hizo zote, motifu ya maisha imetawala. Hili ni suala ambalo Kezilahabi amejishughulisha nalo katika takriban kazi zake zote. Ingawa Rosa Mistika amefanikiwa kupata elimu, anashindwa kukabiliana na matukio ya maisha yake hasa yale yanayohusiana na mapenzi. Hii ni kwa sababu alilelewa kwa kukosa mwelekeo mwema kama tumejadili katika kazi hii.

Riwaya hii ya Kezilahabi ya kwanza inajadili zaidi masuala ya kifalsafa kama vile maana ya maisha na kifo. Rosa anakabiliwa na tatizo la uhuru ambao hajui aufanye nini ndiposa anajiua. Hali ya kukata tamaa aidha imetawala kazi hii.

Katika riwaya ya ***Kichwamaji*** Kezilahabi anaangalia zaidi jinsi Waafrika waliopata elimu ya mfumo wa kikoloni wamekengeuka. Maisha ya wengi

wa wahusika katika riwaya hii hasa Kazimoto, Manase na familia zao yamejaa misukosuko, wivu, kisasi na ukosefu wa utu si kijijini, si mjini. Wahusika wa riwaya hii wanapata mateso makubwa. Sabina (Mkewe Kazimoto) anapata mimba na kuzaa njiti. Mtoto wa Manase anazaliwa na kichwa kikubwa na hata daktari aliyekuwa anamtibu anafariki dunia. Tunaona kuwa maisha ya wahusika hawa ni sitiari inayoelezea mateso yanayompata binadamu katika uchaguzi anaoufanya. Sitiari kama hizi vile vile zimetawala kazi zote za kinathari za Kezilahabi tangu ***Rosa Mistika*** hadi ***Mzingile***.

Riwaya hii ya ***Kichwamaji*** imejadili dhamira ya ufupi wa maisha na suala la kifo, mwelekeo ambao unaonyesha vile mpaka baina ya kifo na uhai ni mwembamba sana.

Katika riwaya ya ***Dunia Uwanja wa Fujo***, jazanda ya fujo ndiyo Kezilahabi ametumia kuelezea maisha. Maisha ya mhusika mkuu ambaye ni Tumaini yamejaa fujo tangu alipokuwa akiishi kijijini hadi anapohamia mjini. Mbali na fujo katika maisha, Kezilahabi pia anashughulikia tatizo la utekelezaji wa mfumo wa Ujamaa nchini Tanzania sambamba na masuala ya kidhanaishi kama vile maana ya maisha, pia utekelezaji wa sera za Azimio la Arusha na siasa ya ujamaa.

Kezilahabi anaonyesha jinsi utekelezaji wa Azimio la Arusha ulivyojaa dhuluma na ufisadi mtupu. Ni dhahiri katika kazi hii kuwa wananchi hawakuchangia sera hizi bali zililazimishwa kwao-kama anavyosema Mamboleo kuwa watu hawakuanzisha wazo la ujamaa bali liliwaangukia watu kama jiwe ikawabidi walibeba.

Aidha kwenye hii riwaya, Kezilahabi ameshughulikia suala la nafasi ya dini katika kutoa suluhisho kwa matatizo yanayowakabili watu. Suala la dini aidha ni mwelekeo wa kidhanaishi ambao upo katika riwaya zake zote hata ***Nagona*** na ***Mzingile.***

Katika kazi hizi zote, Kezilahabi amejikita kwenye masuala ya kifalsafa kama vile maana ya maisha, dini na kifo. Masuala haya ameyashughulikia pia katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** lakini tofauti ni kuwa katika kazi zake za awali amejikita katika muktadha wa historia au hali halisi ya Tanzania tangu uhuru hadi Azimio la Arusha.

Kazi hizi za awali aidha zimeakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisia wa kirasimi kama vile usawiri wa mazingira, usimulizi na uhusika unaokaribiana na ulimwengu halisi. Mtindo huu umebadilika katika ***Nagona*** na ***Mzingile***. Usimulizi si wa moja kwa moja, kuna matumizi mapana zaidi ya sitiari na usawiri wa wahusika na mazingira hauakisi hali halisi ya mazingira ya ulimwengu tunaoujua.

Katika sura ya tatu tumejadili vile Kezilahabi ametumia sitiari na jazanda kusawiri ule ukosefu wa maana katika maisha, vile dini haitoi suluhu kwa matatizo ya watu maisha yamejaa vurumai kama vile jazanda ya ngoma kuu. Hizi sitiari na jazanda zinafumbata vizuri falsafa ya Kezilahabi kuhusu maisha na kuonyesha vile maana ya kazi imo katika lugha kama nadharia ya Umuundoleo inavyosisitiza.

Katika sura ya nne ya kazi hii tumeshughulikia dhana ya mwingilianomatini kwa kulinganisha riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** na riwaya ya mwandishi

wa Mexico ambayo ni ***Pedro Paramo***. Hapa tunaona kuwa riwaya hizi zimeingiliana sana kidhamira na kimtindo. Suala la maisha vile vile limepewa nafasi kubwa katika kazi hizi. Uumbaji wa wahusika na usawiri wa mandhari ambao haufuati kanuni za kirasimi lakini unaoakisi elementi za ki-Usasa na Usasaleo umejitokeza kwa riwaya hizi mbili. aidha masuala ya kidhanaishi kama vile kifo na nafasi ya dini katika maisha ya watu yamejadiliwa pia. Ni dhahiri kuwa mwandishi haandiki kwa ombwe tupu bali ni kweli kuwa matini za kifasihi huingiliana na kuathiriana.

Katika sura ya nne tumeshughulikia sifa za wahusika mashujaa kama ilivyo katika tendi nyingi kote ulimwenguni. Hizi sifa za mashujaa katika kurejelewa zinaonyesha yale majaribio ya kumnusuru mwanadamu au ulimwengu kutoka kwa maangamizi.

Ni dhahiri kuwa Kezilahabi ameivusha fasihi ya Kiswahili hadi kwa mkondo mpya na hivyo kuiendeleza na kuiweka katika fasihi nyingine za kilimwengu.

## 5:2 MAPENDEKEZO

Riwaya za ***Nagona*** na ***Mzingile*** ni kazi ambazo zimefanyiwa uhakiki na wahakiki kadha wa kadha kama tulivyoelezea katika sura ya kwanza lakini bado sehemu nyingi ambazo kwa sababu ya wakati na mada tuliyojikita kwayo haingewezekana kuzijadili zote.

Katika kazi yetu tumeshughulikia elementi chache tu za fani. Fani katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** ni mada pana ambayo inaweza kufanyiwa utafiti peke

yake. Tunapendekeza kuwa wale wahakiki watakaotaka kufanyia riwaya hizi utafiti wanaweza kuzama zaidi kwa mada hii yaani fani.

Aidha elementi zinazohusishwa na Usasa na Usasaleo katika ***Nagona*** na ***Mzingile*** zinaweza kufanyiwa utafiti zaidi kwa mfano msuko wa kazi hii ambapo vitushi havifuatani usimulizi usio wa moja kwa moja na uumbaji wa mandhari na wahusika kwa kutaja tu vichache. Hivi vipengele vinaweza kufanyiwa utafiti zaidi.

## MAREJELEO


Beckett,S (1955): Waiting for Godot, London: Faber and Faber Ltd.

Biebuyck, Daniel K. Matene (1969) The Mwindo /Epic Berkely: University of Califonia Press.

Butler, B (1979): The Myth of a Hero. London: Riden and Company

Cuddon, J.A (1979) A Dictionary of Litrature Terms. London: Andre Deustch Ltd.

Culler, J. (1981) ) The pursuit of signs : Semiotics Literature and Deconstruction, London: Routledge.

Hichens, W (1972) AI Inkishafi, S.A Nassir. Nairobi: Oxford University Press.

International Bible Society (1973 ) Holy Bible . New International Version.

Kezilahabi, E (1971) Rosa Mistika. Nairobi; Kenya Literature Bureau.

__________( 1974) Kichwa Maji. Nairobi: Kenya Literature Bureau

__________( 1979) Gamba la Nyoka. Arusha: East Africa Publication.

__________( 1981) Dunia Uwanja wa Fujo. Arusha; Eastern Africa Publications Ltd.

__________( 1990) Nagona. Dar es Salaam: Dar es Salaam University press.

__________(1991) Mzingile. Dar es Salaam: University Press.

__________(1999) Kaptula la Marx. Dar es Salaam: University Press.

Lawrence,D.H (1958) The Sisters. New York: Grove Printers

Liwenga, G (1981) Nyota ya Huzuni. Dar es Salaam: Hekima Pulishers.

Marquez, G.G (1970) One Hundred years of Solitude. Jonathan Cape: Great Britain

Mbatiah, M (1997) <u>Mienendo mpya katika Uandishi wa Nagona na Mzingile</u> Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mkufya, W.E ( 1999) <u>Ziraili na Zirani</u>. Dar es Salaam: Hekima Pulishers.

Mohamed S.A (2001) <u>Babu Alipofufuka.</u> Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Munga, C.I (1999) <u>Dhana ya Maisha katika Nagona na Mzingile</u> Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mutiso .K. (1985) <u>Hurafa na Uyakinifu katika Hamziya</u>, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mung'ongo, C.G ( 1980) <u>Njozi Iliyopotea</u>. Dar es salaam Tanzania Pulishing House

Ruflo,J .( 1955) <u>Pedro Paramo</u>. New York: Grove Printers Ltd

Sarup, M (1989) An introduction to Postructuralism and Postmodernism. Athens: University of Georgia Press.

Velten, C (1907) Prosa Und Poesie. Berlin: Selbstverlag

Wambui, B. T. (1992) Bonde la Wakati katika Riwaya za Kezilahabi Tasnifu ya M. A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wamitila, K.W ( 1997) Contempus mundi and Carpe diem in Kezilahabis Works- Katika Kiswahili Juzuu 60. Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

_____________(2002) Uhakiki wa fasihi. Misingi na Vipengele vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.

_____________(2002) Bina-Adamu! Nairobi: Phoenix Publishers.

_____________(2003) Kichocheo cha fasihi; Nairobi: Focus Publication Ltd.

Warnock, M (1970) Existentialism . London : Oxford University Press.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION